epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Novemba 17, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0581863
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# MAAFA

• **Jengo** labomoka Kariakoo, watano wafariki, Samia, Waziri Mkuu watoa kauli... *Endelea ukurasa 3*




Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Polisi, Wafanyakazi wa Shirika la Msalaba Mwekundu na wasamaria wema, wakishiriki katika uokoaji, baada ya jengo la ghorofa kuporomoka katika makutano ya mtaa wa Manyema na Mchikichini, jijini Dar es Salaam jana na kusababisha majeruhi wengi. **Picha ndogo:** Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiongozana na Mkuu wa mkoa huo, Albert Chalamila, alipofika kukagua eneo la tukio huku waokoaji wakiwa wamembeba mmoja wa majeruhi. **PICHA ZOTE: IMANI NATHANIEL**








Skani hapa kutembelea chaneli yetu

## RIPOTI MAALUM

# Utumikishaji wa watoto majumbani mfupa mgumu

UKURASA 4

HABARI KITAIFA

# Waziri aonya fikra Kigoma kichaka ajira

**Na Lusungu Helela,** KIGOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu amesema Kigoma si mkoa wa kupatia cheki namba (ajira) na kuhama kwa visingizio vya kuifuata familia au ugonjwa.

Kutokana na hali hiyo , amewataka watumishi kuachana na dhana kuwa mkoa ni wa pembezoni na hauna fursa za kiuchumi.

Sangu aliyasema hayo jana wakati akizungumza na watumishi wa umma wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji, ikiwa ni kliniki ya kimkakati ya kusikiliza na kutafuta ufumbuzi wa kero mbalimbali zinazowakabili watumishi hao.

Alisema kwa kushirikiana na waziri wake, George Simbachawene, wameweka utaratibu wa kufanya klikini hiyo katika mikoa mbalimbali nchini baada ya kuona watumishi wengi wanalazimika kusafiri hadi Dodoma kwa ajili ya changamoto walizo nazo za kiutumishi ambazo zingeweza kutatuliwa papo kwa papo na maofisa utumishi wao.

Sangu alisema kuna dhana imejengeka kuwa mikoa ya magharibi ikiwemo Katavi, Kigoma na Rukwa kuwa ni ya adhabu kwa watumishi ambao wamepangiwa kufanya kazi katika maeneo hayo. Alisema jambo hilo si kweli ambalo hasa baada ya uboreshaji mkubwa wa miundombinu uliofanywa na serikali.

"Kumekuwa na wimbi kubwa la watumishi wa umma mara baada ya kupata ajira huja kuripoti mkoani Kigoma na kuanza taratibu za kuomba uhamisho. Jambo hili si sawa kwani wananchi wa Kigoma nao wanahitaji huduma bora kama wananchi wa Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza," alisisitiza.

Alisema mtumishi wa umma atalazimika kuhama katika mkoa huo endapo atakuwa amekaa miaka mitatu na kuendelea na pia kama atakuwa amepata mtumishi mwenzake wa kubadilishana nae.

Sangu alisema Kigoma ya sasa ni bora kwa sababu Rais Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka mitatu, ametoa zaidi ya Sh. trilioni 11 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ikiwamo barabara na huduma mbalimbali kama vile afya katika mkoa huo.

Alisema kutokana na uboreshaji wa miundombinu hiyo, kwa sasa Kigoma haina tofauti na Dodoma na Arusha kwa kuwa ina kila aina ya fursa pamoja na miundombinu mizuri. Mbunge wa Kigoma Mjini, Kirumbe Ng'enda, alisema Kigoma inahitaji watumishi wachache lakini wenye utayari wa kufanya kazi na si wale walioletwa baada ya kufanya vibaya katika mikoa mingine.

Awali, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Kigoma, Mbwilo Elisante, alisema mkoa unakabiliwa na uhaba mkubwa wa watumishi kutokana na wengi kuhamishwa bila kuletwa mbadala.




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiagana na viongozi mbalimbali katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kuondoka nchini kwenda Rio de Janeiro, Brazil kushiriki Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa nchi Wanachama wa Kundi la G20. Rais, Dk. Samia, amealikwa na Rais wa Brazil, Luiz Inácio Lula da Silva, ambapo pamoja na mambo mengine, atashiriki mijadala inayolenga kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika mapambano dhidi ya njaa na umaskini, kuchochea maendeleo endelevu na matumizi ya nishati mbadala. **PICHA: IKULU**

# Mchengerwa ataja nafasi vyama kusimamisha wagombea

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKATI vyama vya upinzani vikilalama kukatwa kwa wagombea wake, vimesimamisha wagombea 30,977 pekee kati ya nafasi 80,430 zinazowaniwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema idadi hiyo ni sawa na asilimia 38.51 au theluthi moja ya nafasi zinazowaniwa katika uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu,

Mchengerwa alisisitiza kuwa takwimu hizo ni baada ya kukamilika kwa hatua ya rufani za uteuzi, na zilizo sahihi za walioteuliwa zitatolewa baadaye.

"Katika nafasi zinazogombewa, vyama 18 vya siasa vimeweka wagombea katika nafasi 30,977 kati ya nafasi 80,430 sawa na asilimia 38.51, ukiacha Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho kimeweka wagombea katika nafasi zote, katika maeneo ambayo kuna mgombea wa chama kimoja atapigiwa kura ya 'Ndiyo' au 'Hapana', alisema.

Alisema katika nafasi za mwenyekiti wa kijiji zinazogombewa ni 12,280, vyama 18 vya siasa viliweka wagombea katika nafasi 6,060, sawa na asilimia 49.35 ya nafasi hizo.

"Nafasi za mwenyekiti wa mtaa zinazogombewa ni 4,264 ambapo vyama 18 vya siasa viliweza kuweka wagombea katika nafasi 3,281 sawa na asilimia 76.94 ya nafasi hizo.

"Nafasi za mwenyekiti wa kitongoji zinazogombewa ni 63,886 ambapo vyama 18 vya siasa viliweza kuweka wagombea katika nafasi 21,636, sawa na asilimia 33.87 ya nafasi hizo," alisema.

Waziri Mchengerwa alisema hali hiyo ndio uhalisia wa uchukuaji wa fomu za kugombea nafasi mbalimbali kwa vyama vyote vya siasa kabla ya malalamiko ya kuenguliwa kinyume na taratibu. Alisema kutokana na Halmashauri za Wilaya za Kaliua, Nsimbo na Tanganyika kuwa na makazi ya wakimbizi ya Ulyankulu, Katumba na Mishamo na wananchi kuhama kwenye baadhi ya vitongoji kutokana na sababu mbalimbali, maeneo yatakayofanya uchaguzi Novemba 27, mwaka huu, kwa sasa ni vijiji 12,280, mitaa 4,264 na vitongoji 63,886.

**RUFANI ZILIZOKUBALIWA**

Alisema katika halmashauri zote kati ya rufani 16,309 zilizopokewa baada ya muda wa nyongeza wa siku mbili zilizokubaliwa ni 5,589.

Alisisitiza kuwa ilizingatiwa dosari ambazo zilisababisha kutoteuliwa kwao hazikuwa kubwa zinazoathiri matokeo yaliyokusudiwa na kanuni.

**WAGOMBEA KUTOTEULIWA**

Kuhusu dosari zilizosababisha baadhi ya wagombea kuenguliwa alizitaja kuwa ni kukosa sifa ya uraia wa Watanzania, kujidhamini wenyewe, kutojiandikisha kwenye daftari la wapigakura wa Serikali za Mitaa na wengine kuwa chini ya umri wa miaka 21.

Alisema wagombea wengi ambao hawakuteuliwa ni kwa mujibu wa vigezo vya kikanuni na kulikuwa na nafasi ya kuweka pingamizi dhidi ya mgombea au dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi na rufani endapo mlalamikaji asingeridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi dhidi ya pingamizi alilowasilisha.

**UFAFANUZI WA TUHUMA**

Alisema kuna viongozi vya vyama vya upinzani wametoa tuhuma ambazo baada ya ufuatiliaji waligundua hazikuwa na ukweli na zililenga kuleta taharuki na kuchafua mchakato wa uchaguzi uliokuwa unaendelea vizuri.

"Baada ya uteuzi wa wagombea Novemba 8, 2024, aliyekuwa Diwani wa Ubungo, Boniface Jacob alitoa tuhuma kuwa katika Mkoa wa Dar es Salaam wenye mitaa 636 wamekata majina ya wagombea wa CHADEMA 571 na yamebaki majina 45 tu na kuwa watendaji wa kata wamepewa maelekezo ya kutowateua wagombea wa CHADEMA, tuhuma hizi si za kweli," alisema.

Alisema halmashauri za mkoa huo zina jumla ya mitaa 564 na sio 636 kama ilivyotajwa, ambapo katika mitaa hiyo CCM walichukua fomu mitaa yote 564 na CHADEMA walichukua fomu katika mitaa 437 kati ya mitaa 564 na waliteuliwa 282 na sio 45 kama ilivyosemwa.

"ACT walichukua fomu katika mitaa 219 na walioteuliwa 144, walioteuliwa na CUF walichukua fomu katika mitaa 148 na waliteuliwa 93.

"Kwa mara nyingine alieleza kuwa katika vijiji 32 vilivyopo katika Wilaya ya Rufiji wanachama wa CHADEMA wameondolewa wote, ni vyema umma ujue Wilaya ya Rufiji ina vijiji 38 na katika vijiji hivyo kuna vitongoji 178.

"Katika vijiji vyote 38 CHADEMA waligombea kijiji kimoja katika vitongoji 178, CHADEMA waliweka wagombea wawili sio kweli kusema kuwa katika Jimbo la Rufiji wagombea wote wa CHADEMA wameondolewa na ni vyema kuueleza umma kuwa hawakuweka wagombea katika maeneo wanayowataja," alisema.

Kuhusu kufungwa ofisi siku ya kuwasilisha mapingamizi, Mchengerwa alisema ofisi yake ilifuatilia katika maeneo hayo na mengine nchini na kubainika kuwa hazikufungwa na wagombea walifanikiwa kupeleka pingamizi zao katika maeneo hayo.

Aliwasihi wadau wa uchaguzi huo kuacha kufanya propaganda ambazo hazina ukweli na zinazoleta taharuki inayohatarisha amani iliyopo.

Alisisitiza kuwa uchaguzi unazingatia Sheria na Kanuni za Uchaguzi na sio huruma ili kuhakikisha uchaguzi huo unaendelea kufanyika kwa misingi ya haki, usawa na utawala bora.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations @guardian.co.tz*

HABARI KITAIFA

## Mpango anadi fursa uwekezaji Tanzania

**Na Benny Mwaipaja,** BAKU, AZERBAIJAN

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameihamasisha sekta binafsi na wadau wengine wa maendeleo wa kimataifa kuchangamkia fursa za uwekezaji zinazopatikana Tanzania. Miongoni mwa fursa hizo ni uchumi wa buluu kwa faida za kiuchumi na hifadhi ya mazingira ikiwa ni sehemu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Mpango alitoa wito huo katika kotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji, wakati akifungua mkutano wa kunadi fursa za uwekezaji katika sekta ya uchumi wa buluu zilizoko Tanzania.

Mkutano huo ulioandaliwa na serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Uchumi wa Buluu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ulifanyika pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) unaofanyika katika mji wa Baku, Azerbaijan.

Mkutano huo ulihudhuriwa na viongozi waandamizi kutoka Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, Shirika la Chakula Duniani (FAO), Shirika la Hifadhi ya Maliasili (IUCN) na mashirika mengineyo. Dk. Mpango alisema ni muhimu kuwekeza katika shughuli endelevu za uchumi wa bluu na miradi ya kurejesha, kama vile marejesho ya mikoko, miamba ya matumbawe na bahari, uhifadhi wa maeneo ya mvua na kilimo cha mwani kinaweza kuongeza utenganishaji wa kaboni na kusaidia malengo ya kukabiliana na athari hasi za mabadiliko ya tabianchi kama ilivyoainishwa katika Itifaki ya Kyoto na Mkataba wa Paris.

Aliyataja maeneo ya uwekezaji kuwa ni pamoja na uchimbaji wa madini, uvunaji wa mafuta na gesi, ujenzi wa bandari kavu, uvuvi mkubwa katika kina cha Bahari katika eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 223,000. Alisema uwekezaji huo utachangia kukuza uchumi wa nchi na wawekezaji, lakini pia utakuza ajira kwa makundi ya watu wanaojihusisha na shughuli mbalimbali baharini na vyanzo vingine vya maji.

Dk. Mpango alibainisha kuwa Tanzania imeendelea kujenga miundombinu wezeshi ya kurahisisha ufanyajikazi katika sekta ya uchumi wa buluu ikiwemo kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya Bahari ili kuyaongezea thamani ikiwemo zao la mwani na kujenga viwanja vya ndege na bandari visiwani Zanzibar na mikoa ya kusini.

Wakizungumza katika mkutano huo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Riziki Shemdoe, na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Zahor Kassim El Kharousy, walieleza umuhimu wa uwekezaji katika sekta ya uchumi wa buluu ikiwemo upatikanaji wa kodi pamoja na maendeleo ya watu.

Zaidi ya watu 200 toka mataifa mbalimbali wakiwamo viongozi waandamizi kutoka Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya, FAO, IUCN na mashirika mengine waliahidi kuendelea kusaidiana na Tanzania kwenye upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya masuala ya kukabiliana na madhara ya mabadiliko ya tabianchi kwenye sekta ya uvuvi Tanzania.

# Maafa jengo laporomoka, laua na kujeruhi

**Na Waandishi Wetu**



Waokoaji wakiendelea na kazi ya kuwaondoa majeruhi katika eneo la tukio, baada ya jengo la ghorofa kuporomoka katika makutano ya Mtaa wa Manyema na Mchikichini, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

TAHARUKI ilizuka jana asubuhi baada ya jengo la ghorofa nne kuporomoka Kariakoo, jijini Dar es Salaam na hadi jioni aliyefariki dunia alikuwa mtu mmoja na wengine 40 kujeruhiwa.

Tukio hilo lilitokea kati ya Mtaa wa Congo na Mchikichi, baada ya jengo hilo lenye maduka ya biashara kuporomoka na kufukia watu na mali zilizokuwapo. Mashuhuda wa tukio hilo, walisimulia waathirika walivyopitia nyakati ngumu wakipiga kelele kuomba kuokolewa baada ya kufukiwa na vifusi vya jengo hilo ambalo inadaiwa chini lilikuwa likijengwa.

Mmoja wa watu waliokuwa ndani ya jengo hilo, mama mwenye watoto wawili, alionekana akilia na kumwomba Mungu kuwanusuru na kifo. Baadhi walionekana wakiwapigia simu ndugu zao na wako walioongea nao kwa saa kadhaa na baadaye hawakupatikana tena.

**HALI ILIVYOKUWA**

Kasi ya uokoaji ilikuwa ndogo hadi ilipotimu saa 4:48 asubuhi Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilipowasili na kuanza uokoaji ikiwamo kuwapelekea mitungi ya gesi watu waliokuwa chini ya ghorofa.

Ilipofika saa 6:30 mchana, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) lilifika kuongeza nguvu za uokoaji, hali iliyoibua shangwe kutoka kwa wananchi ambao waliwapokea kwa kuwapigia makofi.

Baada ya kuporomoka kwa jengo hilo, shughuli mbalimbali sokoni hapo zilisimama kwa muda kati ya mitaa ya Mchikichi na Congo. Baadhi ya wataalamu walioongoza uokoaji ni pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Muhimbili, Prof. Mohamed Janabi.

**SHUHUDA MBALIMBALI**

Wakala wa usafirishaji mizigo inayotoka China, Kabila Juma, alisimulia kuwa alishuhudia ghorofa hilo likiporomoka na halikuporomoka ghafla bali lilianza taratibu.

Alisema baadhi ya watu waliokuwa ndani ya jengo hilo wakati likiporomoka, walitoka na wale waliokuwa maduka ya chini, wengi wao walishindwa kutoka kwa wakati, hivyo mara moja walianza uokoaji.

Ally Salehe anayejishughulisha na ubebaji mizigo, alisema katika jengo hilo kulikuwa na ujenzi unaendelea kwenye maduka ya chini.

**RAIS SAMIA**

Kutokana na maafa hayo, Rais Samia Suluhu Hassan aliuagiza uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na Idara ya Menejimenti ya Maafa kufanya kila linalowezekana kufanikisha uokoaji na tiba kwa majeruhi.

"Wakati hilo likiendelea na tunamwomba Mwenyezi Mungu awape pona ya haraka majeruhi. Tuwaombee pia utulivu na subira ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wenzetu wanaotafuta riziki zao katika eneo hili muhimu kibiashara nchini ambao kwa namna mbalimbali wameathiriwa na ajali hii," alisema.

**ATEMBELEA MAJERUHI**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, jana alifika eneo la tukio na baadaye kuwatembelea majeruhi Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kuviagiza vyombo vyote vya usalama kuhakikisha watu wote waliokwama ndani ya jengo hilo wanaokolewa na mali zinalindwa.

Alisema katika ajali hiyo mtu mmoja ameripotiwa kufariki dunia hadi jana jioni na Muhimbili walikuwa wamepokea jumla ya majeruhi 40 ambapo kati yao, 33 walitibiwa na kuruhusiwa.

Katika eneo la tukio, Majaliwa alisema majeruhi wengine wamepelekwa Hospitali za Rufani za Mwananyamala, Amana na Temeke.

Alitumia fursa hiyo kuwahakikishia Watanzania kuwa kazi kubwa ya uokoaji inaendelea na vyombo vyote vya ulinzi na uokoaji vipo katika eneo hilo, hivyo amewataka waendelee kuwa na subra.

Majaliwa pia alimwelekeza Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Dk. Jim Yonazi, kusimamia uchunguzi ili kubaini chanzo cha ajali hiyo.

"Wataalam mnaohusika na masuala ya ujenzi fanyeni ukaguzi wa ujenzi wa majengo unaoendelea," aliagiza nakusisitiza kuwa kazi ya uokoaji itaendelea hadi kuhakikisha anatolewa hadi mtu wa mwisho.

"Nikiwa hapa nimeona mtu mmoja ametoka na amesema wenzake wapo chini," alisema. Pia aliagiza kwa wanaojenga majengo mapya katika eneo hilo kuhakikisha yanakuwa na ubora ili kuepuka matukio kama hayo kujitokeza tena. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila alisema: "Nitoe rai kwamba muda huu si wa kulaumiana kwamba nani amesababisha hili tatizo.

Ni muda wa kuokoa uhai wa wenzetu." Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema jeshi hilo limetoa askari wa kutosha kuimarisha ulinzi na usalama wa mali za watu walioathirika na atakayebainika kuziiba atachukuliwa hatua.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Soko la Kariakoo, Martin Mbwana, alisema ni mapema kujua idadi ma maduka yaliyokuwapo ndani ya jengo hilo pamoja na mali zilizopotea.

**AQRB WAELEZA KISHERIA**

Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Edwin Nnunduma, alisema sheria ya ujenzi inazuia jengo kutumika kabla halijakamilika.

"Ili jengo litumike, linapata vibali kutoka halmashauri. Tunajua lilikuwa linatumika huku linajengwa. Watu ambao wanaweza kutoa maelezo mazuri ni halmashauri. Hatujui lilikuwa likitumika katika hatua gani.

Lingekuwa liko kwenye ujenzi, sisi tungekuwa tuna taarifa za nini kimetokea," alisema.

Alisema bodi hiyo inatuma timu yake kuchunguza ili kubaini chanzo cha ajali hiyo na ndipo watatoa taarifa na ushauri wa kitaalamu kwa umma.

**HAKI ZA WAATHIRIKA**

Wakili wa Mahakama Kuu, Jebra Kambole, alisema waathirika wa ajali hiyo wanaweza kudai fidia kwa mmiliki.

"Kama mmiliki alitakiwa ahakikishe eneo lake lote linakuwa salama, kwa kuzingatia ubora wa jengo na kila kitu.

Hii ni kanuni ya occupiers liability (mzigo kwa wamiliki) ambayo mmiliki wa eneo anawajibika moja kwa moja. Fidia haijaainishwa, inategemea na madhara aliyopata mtu," alisema.

**MATUKIO KAMA HAYO**

Desemba 21, 2022, katika Kijiji cha Sembeti Marangu, mkoani Kilimanjaro, jengo la ghorofa ambalo ujenzi wake ulikuwa ukiendelea, liliporomoka na kusababisha vifo vya mafundi watano na majeruhi kadhaa.

Mwaka 2006 huko Chang'ombe, Dar es Salaam, jengo la Hoteli ya Chang'ombe Village (sasa Tanzania Hotel), liliporomoka na kuua watu wanne. Pia mwaka 2013, ghorofa lingine liliporomoka katika Mtaa wa Indira Gandhi, Dar es Salaam na kuua takriban watu 36, chanzo kikitajwa kuwa ujenzi usiozingatia utaalam.

Hadi gazeti hili linakwenda mtamboni shughuli za uokoaji zilikuwa zikiendelea maeneo hayo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations @guardian.co.tz***

# Utumikishaji wa watoto majumbani mfupa mgumu

**Na Waandishi Wetu**

MSAIDIZI wa ndani ni hitaji la kila mwanamke ambaye yuko katika shughuli za kiuchumi. Pamoja na umuhimu huo, kuna utumikishaji mkubwa wa watoto chini ya miaka 18, umri ambao ni wa mtoto kuwapo katika mfumo wa elimu.

Licha ya serikali kuweka mazingira wezeshi kwa mtoto kusoma bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha sita, lakini uchunguzi wa Nipashe umebaini kuwapo kwa changamoto hiyo katika miji na majiji.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Amina Makilagi, anasema watoto saba hadi 10 walio chini ya miaka 14, husafirishwa kila mwezi kutoka wilayani Ngara kupelekwa jijini Mwanza kwa ajili ya kufanya kazi za ndani.

Anasema hali si nzuri hivyo kuwataka wadau pamoja na jamii kwa ujumla kushirikiana kwa karibu kuhakikisha hali hiyo inadhibitiwa, ili watoto hao wapate fursa ya elimu.

Mtoto mwenye umri wa miaka 12 (jina limehifadhiwa) mkazi wa Ngara mkoani Kagera, anasimulia namna ambavyo hakubahatika kwenda shule licha ya kuwa na matamanio hayo.

Anasema miaka miwili nyuma akiwa na miaka 10, alimwuliza baba yake sababu za kutokwenda shule kama watoto wengine anaocheza nao kila siku.

Tofauti na matarajio yake, majibu aliyopewa ni kwamba hakuna ambaye ataweza kumtafutia mahitaji ya shuleni wakati chakula ndani ya familia yao upatikanaji wake ni shida.



Pamoja na juhudi mbalimbali za serikali za kuhakikisha kila mtoto anapata elimu ya msingi, bado kuna idadi ya watoto wenye umri chini ya miaka 14 walioajiriwa kwenye kazi za nyumbani, zinazowafanya kukosa haki ya kupata elimu na haki ya kulelewa kama watoto. **PICHA: MTANDAO**

"Niliambiwa nisubiri atakuja mtu kunipeleka mjini kufanya kazi za ndani. Baada ya siku tatu alikuja mgeni nyumbani kwetu, aliongeza na baba nikaambiwa nijiandae nakwenda mjini kufanya kazi za ulezi wa watoto na shughuli za ndani," anasimulia mtoto huyo.

Binti huyo ambaye ni mwenyeji wa kijiji cha Kumnazi, kata ya Kanazi, anasema alipandishwa gari la kwenda Bukoba mjini na aliambiwa atapokewa na mwanamke ambaye ataishi naye huko.

Naye binti wa miaka 14 kutoka Ukerewe mkoani Mwanza, mwenye simulizi tofauti na mwenzake, anasema alipomaliza shule ya msingi, wazazi wake walimwambia anakwenda mjini kufanya kazi ili awatumie fedha kijijini kwa sababu maisha yao ni duni.

"Changamoto ninayopata hapa ni muda wa kupumzika ambapo huwa ni usiku tu tofauti na nilivyokuwa nyumbani. Kazi zangu ni kufua nguo za familia nzima, kufanya usafi na kupika chakula," anasema.

Binti wa miaka 15 ambaye mwaka huu alipaswa kuwa kidato cha pili, anasema aliacha shule akiwa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Lubugu, wilayani Magu na kukimbilia kuuza baa akiamini maisha yake yatakuwa bora.

"Wakati ninasoma mwalimu wangu alinipenda kutokana na bidii na utiifu, ghafla nikabadilika na kutoroka nyumbani kutafuta kazi na ndipo nilipoangukia kazi ya uuzaji wa baa katika eneo la Ihayabuyaga, Magu," anasimulia.

Binti huyo anasema changamoto anazokutana nazo kazini ni utumikishwaji kingono, kufukuzwa na wamiliki wa baa na wakati mwingine kukosa makazi, hivyo kulazimika kuzunguka mtaani na inapofika jioni kuomba hifadhi na nyakati nyingine hukosa chakula.

"Nyumbani hawajui changamoto ninazopitia. Wanajua nimefanikiwa kupata kazi nzuri. Wakati mwingine baba uniomba fedha. Ninapitia wakati mgumu sana, ninatamani kurudi nyumbani, lakini ninaogopa mitaonekanaje" anasema.

Sara John (17) ambaye alitarajia kuwa kidato cha nne mwaka huu, anasema alikatisha masomo akiwa kidato cha pili baada ya kupata ushawishi kutoka kwa marafiki kuwa Dar es Salaam kuna nafasi nyingi za kazi, lakini alivyokwenda alikutana na hali tofauti na alivyoelezwa awali.

**SHERIA INASEMAJE**

Wakati watoto wakisimulia madhira yanayowasibu, Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 kifungu cha 9(1) imeainisha wajibu wa mzazi ikiwamo kumopatia mtoto haki ya kuishi, utu, heshima, mapumziko, uhuru, huduma za afya, elimu na malazi.

Lakini bado wazazi wamejificha katika kifungu kidogo cha (2) cha sheria hiyo kisemacho, haki hiyo itazingatia mwongozo na uwezo wa mzazi, mlezi au ndugu.

Mkazi wa Kijiji cha Minkoto mkoani Geita, Veronica Yombo, anasema tatizo la watoto hao kuishia kutumikishwa ni baadhi ya watu wa mjini kutumia kigezo cha umaskini wa familia za watoto hao kwa kuwarubuni kwa fedha na kuchukua mabinti zao wenye umri wa kwenda shule kufanya kazi za ndani.

Mkazi wa Bukoba mjini ambaye ni mwajiri wa mtoto kutoka Ngara (jina tunalo), anasema: "Ili kupata wasaidizi wa ndani, kuna wakati hutumia madalali, ndugu au jamaa wa dada hao. Pia wako wanaopita mtaani kuomba kazi kwa malipo ya siku."

Anasema wadada wanaowapenda ni wenye umri mdogo chini ya miaka 18 kwa sababu sio wasumbufu katika kazi na wakiagizwa wanafanya.

Omary Ibrahim, mkazi wa Nyamagana jijini Mwanza, anasema suala la ajira kwa watoto ni jambo ambalo halifuatiliwi na kuchangia watoto kutumikishwa.

"Ukihitaji mfanyakazi unapiga simu au kutoa tangazo mtandao unaletewa. Mara nyingi ninamwona mke wangu anaagiza na analetewa tunaishi nao japokuwa si wadogo, lakini changamoto huwa hatupajui kwao zaidi tunawasiliana na wazazi na ndugu zake kwa njia ya simu ninajua ni hatari," anasema. Ofisa Ustawi Jamii wa Manispaa ya Bukoba, Japhet Kanoni, anakiri kupokea kesi za namna hiyo mara kwa mara hasa kwa watoto wanaokuwa wamepishana na waajiri wao kisha kufukuzwa kazi.

Anasema wanapohojiwa baadhi husema katika familia wanazotoka hazina uwezo kuanzia makazi, chakula na huduma nyingine muhimu.

Kanoni anasema kutambua kama binti wameajiriwa katika familia ni vigumu, hivyo huwatambua na kuwasaidia pale wanaposhindwana na waajiri wao na baada ya manyanyaso.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Minkoto iliyoko Chato mkoani Geita, Gilbert Kayena, anakiri kuwapo kwa tatizo hilo. Anasema wengi wao hukimbilia mijini wengine kwenda kufanya vibarua kama kulima na kuchunga ng'ombe.

"Tatizo hili lipo lakini siyo kubwa. Wazazi wameanza kuelimika na kujitambua, wawakubali kuwatoa vijana wao kwenda kufanya kazi mijini, mashambani au kuchunga mifugo," anasema Kayena.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mikonto, Jerome Nestory, anasema kijiji hicho kinakabiliwa na uhaba wa shule na madarasa, huku kikiwa na idadi ya wakazi 8373 kati ya hao nusu ni watoto.

Anasema watoto hushindwa kuendelea na masomo kutokana umbali wa shule uliko au kutumikishwa katika umri mdogo.

Aliyekuwa Mwenyekiti wa Majengo Kata ya Mkolani jijini Mwanza, Ramadhani Musabi, anataja mbinu ya kutokomeza tatizo hilo ni kuwadhibiti madalali katika vituo vya mabasi na stendi, ambako ndio njia kuu ya kuwasambaza kwa ajiri.

***IMEANDALIWA na Vitus Audax, Rose Jacob, Neema Emmanuel (MWANZA), Restuta Damian (BUKOBA), Judith Julius (NGARA).***

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Mabaki ya mabati, baada ya vibanda 25 vikiwa na mali, kuteketea kwa moto katika Soko la Mbamba Bay, wilayani Nyasa, mkoani Ruvuma, usiku wa kuamkia jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahamasishwa upimaji kisukari kujua hali zao

**Na Romana Mallya**

WAKATI Tanzania ikiungana na dunia kuadhimisha Siku ya Kisukari Duniani mwaka huu, kilio kikubwa cha wadau ni ongezeko la ugonjwa huo huku wasiojua kama wana tatizo wakiwa asilimia 78.

Mwenyekiti wa Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), Prof. Andrew Swai, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho hayo yaliyofanyika kwa kuhamasisha jamii kupenda kuushughulisha mwili kwa kufanya mazoezi.

Prof. Swai ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wagonjwa wa Kisukari Tanzania (TDA), baada ya kushiriki mazoezi ya kutembea, alisema hesabu alizofanya kwa wenye ugonjwa wa kisukari wanaojijua ni asilimia 22 tu.

Alisema asilimia iliyobaki hawajui na baada ya kufikishwa hospitalini tayari huwa katika hali mbaya.

"Asilimia tisa ya Watanzania wana ugonjwa wa kisukari na kuwatibu ni kazi kubwa, huku asilimia 26 wana presha iliyozidi na asilimia 34 wamenenepa mno.

Nilifanya mahesabu kuona wenye ugonjwa wa kisukari ambao wanajijua ni asilimia 22 tu, wengine hawajijui mpaka wanapokwenda hospitali wakiwa katika hali isiyo nzuri," alisema.

Prof. Swai alisema asilimia 60 wenye kisukari wana presha na wanaojijua wana presha ni asilimia 30 na wengine ni mapaka wapate kiharusi ndipo wajue wana matatizo hayo.

"Watu wengi wenye presha hawana dalili. Ukiamua kuwatibu tu wale wanaojijua kwa dawa za kuanzia utahitaji robo yote ya bajeti ya afya ndiyo maana ukienda hospitalini unakuta dawa hakuna. Ni tatizo kubwa kwa sababu uwezo wa kutibu hakuna.

"Nchi zilizoendelea Norway na Uingereza wanatumia Dola za Marekani 4,000 kwa mwaka kutibu matatizo haya. Sisi tunatumia Dola 40. Pato la Taifa ni Dola 1,000 ambayo ni robo ya fedha ambazo zinatumiwa nchi za Ulaya kwa ajili ya tiba peke yake," alisema.

Alisema ili kuepuka kupata maradhi hayo ndio maana wanasisitiza ufanyaji mazoezi, kula mlo kamili, kuacha pombe na sigara.

Prof. Swai alisema miaka hadi 1987 kulikuwa na asilimia chini ya moja waliokuwa na ugonjwa wa kisukari, chini ya asilimia tano waliokuwa na presha iliyozidi, chini ya asilimia tano ya wenye unene uliozidi, lakini hivi sasa wenye unene uliozidi ni asilimia 35.

Alisisitiza kwamba mazoezi ni shughuli zozote zinazoshughulisha mikono, miguu, moyo na mapafu.

"Saratani imeongezeka kwa mwaka tunaona wagonjwa zaidi ya 40,000 wenye ugonjwa huu. Huko nyuma haikuwa hivyo tulivyoanza na Ocean Road ilikuwa hospitali ya kinamama na saratani, ile wodi ilitosha lakini kwa sasa tumeongeza jengo nalo halitoshi.

"Tunahitaji watu wajue nini cha kufanya kuepuka haya matatizo, kula mlo kamili pasipo kuongeza chumvi zaidi ya kijiko kimoja cha chai kwa siku na sukari usizidishe vijiko vitano vya chai kwa siku.

"Mafuta usizidishe kidole gumba kwa siku na tunasisitiza ufanyaji wa mazoezi, kupumzika vya kutosha angalau saa saba kila siku ili mwili kujitengeneza ulikoharibika. Vichocheo vingi hutengenezwa usiku," alisisitiza.

Mtaalam wa Afya na Mazoezi kutoka TANCDA, Dk. Waziri Ndonde, alisema Novemba 14 ya kila mwaka ni maadhimisho ya kisukari duniani na mara nyingi huadhimishwa kwa matembezi ili kutoa wito wananchi kwamba ufanyaji mazoezi ni muhimu katika mapambano hayo.

"Bahati nzuri mwaka huu yamefanyika kukiwa na tamko la serikali la kutumia maeneo haya ya Daraja la Tanzanite hadi Coco Beach kila Jumamosi kufanya mazoezi. Siku hii huadhimishwa na wiki ya magonjwa yasiyoambukiza ambayo huwa na shughuli mbalimbali na kwa mwaka huu unafanyika upimaji wa afya Dodoma na hata hapa lipo gari maalum linalotoa huduma hiyo," alisema.

Alisema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu ilikusanya watu kwa kuhusisha wizara karibu 18 kuangalia namna gani wanaweza kufanya kazi pamoja ili kuhakikisha Watanzania hawapati magonjwa hayo.

Kuhusu mwitikio wa wananchi katika mazoezi, Dk. Ndonde alisema, bado ni mdogo na kutoa wito kila mtu kulingana na eneo aliko ashiriki ili kupambana na magonjwa hayo yanayotumia gharama kubwa kuyatibu.

Dk. Ndonde alisema mazoezi wanayopaswa kufanya wagonjwa wa kisukari ni ya kutembea, kuogelea na kuruka kamba.

"Lakini wagonjwa wa kisukari huwa na maangalizo kutoka kwa watalaam wao wanaowahudumia ni muhimu kuwasilikiza kile wanachoelezwa katika kliniki zao. Ni dalili gani wanaziona wakati wakifanya mazoezi ama waache au wabadilishe mtindo wa mazoezi," alisema.

Alishauri mgonjwa wa kisukari akiwa anafanya mazoezi ya kutembea ni muhimu kuwa na vitu mfano pipi ili anapohisi sukari imeshuka atumie na anaposikia kizunguzungu au kuishiwa nguvu hushauriwa kuyacha mara moja na kupima sukari yake.

"Kwa ujumla ushauri wa kitalaam ni watu wapime afya kabla ya kufanya mazoezi hiki ni kitu cha msingi, kwa sababu kuna ambao wana kisukari lakini hawajijui, anafanya mazoezi baadaye anadondoka barabarani. Pima na ufuate maelekezo ya mtaalam," alisema.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations @guardian.co.tz*

## Soko la Mbambabay lateketea kwa moto

**Na Gideon Mwakanosya,**
NYASA

SOKO kuu la Mji Mdogo wa Mbambabay katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, mkoani Ruvuma limeteketea kwa moto alfajiri ya kuamkia jana.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Nyasa ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Kisare Makori, alisema tukio hilo usiku wa kuamkia jana kati ya saa tisa na nusu na saa kumi alfajiri.

Alisema taarifa za awali ni kwamba, moto huo umeteketeza vibanda 25 vya wafanyabiashara katika eneo la soko hilo, ukianzia katika mojawapo ya kibanda na kusambaa zaidi.

Makori alisema moto huo ulizimwa kwa msaada uliotolewa na askari polisi, wafanyakazi wa bandari ambao walifika na boza lenye maji na kuuzima.

Alilipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Nyasa kwa kazi waliyoifanya kutokana na moto huo kuathiri moja ya nguzo hivyo kuzima umeme ili kutoleta madhara zaidi.

"Kwa bahati mbaya wilaya ya Nyasa hakuna gari la zimamoto, ninashukuru uongozi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, Twi la Mbambabay kwa kuona umuhimu wa kuleta boza la maji ambalo limezima moto huu ambao tayari vibanda 25 vya wafanyabiashara vilikuwa vimeteketea," alisema.

Alisema chanzo cha tukio hilo bado hakijajulikana licha ya kuwa wataalamu wameagizwa kufanya uchunguzi wa kina ili kukibaini.

Diwani wa Mbambabay, Ajali Hasan, aliiomba serikali kuona umuhimu wa kuwasiliana na taasisi za fedha zikiwamo benki ili waweze kuona namna ya kuwasaidia wafanyabishara hao ambao wengi wao walichukua mikopo taasisi za fedha.

Kadhalika aliiomba serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuchukua hatua za haraka za kuweka askari wa kutosha pamoja na magari ya zimamoto katika wilayani Nyasa ambako kuna Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, hospitali, taasisi za fedha, bandari, na hoteli za kitalii.

Baadhi ya masoko yaliyowahi kuteketea ni pamoja na soko la Mwanjelwa (Septemba 16, 2011), soko la Sido (Agosti 20, 2017) yote ya jijini Mbeya.

Mengine ni soko kuu la Kariakoo lililoko jijini Dar es Salaam (Julai 13, 2021) na la Mchikichini, soko la Njombe (Aprili 2, 2023) na masoko mawili huko Songea Mjini.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii izingatie ushauri wa wataalamu kuepuka kisukari

**NOVEMBA** 14 kila mwaka, ni Siku ya Kisukari Duniani. Siku hii huadhimishwa na nchi zote wanachama wa Umoja wa mataifa kwa lengo la kuelimishana na kuhusu ukubwa wa tatizo na ni njia gani zinapaswa kuchukuliwa ili kukabiliana nalo.

Katika maadhimisho ya mwaka huu, kaulimbiu ilikuwa "Kuvunja Vikwazo, Kuziba Mapengo". Lengo la kaulimbiu hiyo lilikuwa kuongeza uwajibikaji katika kupunguza madhara ya kisukari na kuhakikisha watu wote wanaobainika kuwa na ugonjwa huo, wanapata huduma kwa usawa, bei nafuu na matibabu ya huduma za viwango.

Takwimu mpya zinaonesha kuwa tatizo la kisukari limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka, hivyo kuonesha kuwa ni moja ya majanga yanayoiandama dunia kiafya. Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), watu milioni 830 wana ugonjwa huo ikikadiriwa kuwa kwa mwaka, zaidi ya watu milioni nne hupoteza maisha kwa sababu ya ugonjwa huo.

Kwa Afrika, takwimu za Shirikisho la Kimataifa la Kisukari (IDF) zinaonesha kuwa zaidi ya watu milioni 24 wenye umri kati ya miaka 20 na 79 wana ugonjwa huo. Sababu kubwa ya ongezeko hilo inabainishwa kuwa asilimia 54 ya watu hawajajitokeza kupima afya na kubainika kama wana tatizo hilo.

Hali kwa Tanzania nayo si ya kuridhisha kwa kuwa taarifa zinaonesha kuwa kila mwaka idadi ya wagonjwa imekuwa ikiongezeka. Mwaka 1984, kwa mfano, chini ya asilimia moja ya Watanzania wote waligundulika kuwa na ugonjwa huo. Idadi iliongezeka mwaka 2012 na kufikia asilimia 9.1 na mwaka 2021, kwa mujibu wa Benki ya Dunia (WB), iliongezeka hadi kufikia asilimia 12.3.

Hali hiyo pia inaonesha kuwa tatizo linazidi kuwa kubwa kutokana na watu kutokupima na kujua afya zao. Kwa mujibu wa Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA), asilimia 78 ya watu hawajui kama wana matatizo hayo.

Mwenyekiti wa TANCDA, Prof. Andrew Swai, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Kisukari Tanzania (TDA) aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho hayo yaliyofanyika kwa kuhamasisha jamii kupenda kuushughulisha mwili kwa kufanya mazoezi kuwa watu wanaojijua kuwa na ugonjwa wa kisukari ni asilimia 22 tu huku asilimia iliyobaki wakiwa hawajui na baada ya kufikishwa hospitalini tayari huwa katika hali mbaya.

Sababu kubwa zinazochangia kuongezeka kwa wagonjwa ni mtindo wa maisha kwa watu wengi kutokufanya mazoezi na ulaji wa vyakula usio sahihi kama inavyoshauriwa na wataalamu wa afya. Hali hiyo imesababisha watu kuwa na afya isiyo nzuri. Inaelezwa kuwa kutokana na hali hiyo, asilimia 26 ya watu wenye kisukari wana presha iliyozidi na asilimia 34 wana unene uliopitiliza.

Kutokana na kuongezeka kwa tatizo hilo, ni wakati mwafaka sasa kwa Watanzania, wale ambao hawajajua hali ya afya zao, kujitokeza na kupima ili kutambua kama wana ugonjwa huo au la. Iwapo watabainika, waanze kutumia dawa kama watakavyoelekezwa na madaktari pamoja na kuhudhuria kliniki. Wale ambao watabainika kuwa bado wako salama dhidi ya kisukari, wazingatie mashrti ikiwamo kufanya mazoezi na kuepuka kutumia vyakukla na vinywaji ambavyo huchangia kupata maradhi hayo.


Aidha, jamii inapaswa kuzingatia maelekezo ya madaktari ikiwamo kuepuka kupatwa na kisukari na magonjwa mengine yasiyoambukiza kama vile kula mlo kamili pasipo kuongeza chumvi zaidi ya kijiko kimoja cha chai kwa siku na sukari vijiko vitano vya chai kwa siku.

Matumizi ya mafuta kwa kiasi kikubwa kwenye chakula pia ni sababu, hivyo jamii inapaswa kuzingatia hilo kwa kutumia kiasi kidogo ili kuepuka kupata matatizo ya lehemu mwilini, shinikizo la damu na maradhi ya mfumo wa kupumua.

Kubwa zaidi jamii inapaswa kuzingatia kufanya mazoezi ya mara kwa mara kama inavyoshauriwa kwa kufanya hayo, ushindi dhidi ya kisukari utakuwa mkubwa na jamii itaishi bila hofu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hujuma hizi reli ya SGR zidhibitiwe mapema

Na Sabato Kasika

**SERIKALI** imejenga reli ya kisasa kuanzia Dar es Salaam kwenda mikoa ya Kigoma na Mwanza, tayari awamu ya kwanza ya ujenzi huo ikiwa imekamilika hadi Dodoma ambako sasa abiria wanasafiri na treni hiyo.

Reli ya kisasa na ya kwanza Afrika mashariki na kati itakayokuwa na uwezo wa kupitisha treni zinazoendeshwa kwa nishati ya umeme na yenye mwendo kasi usiopungua kilometa 160 kwa saa.

Hata hivyo, cha kushangaza ni kwamba wakati treni ikiendelea kutoa huduma ya usafiri, wapo baadhi ya Watanzania wanaotuhumiwa kuharibu na kuiba miundombinu ya reli.

Hivi karibuni Jeshi la Polisi mkoani Dodoma lilitangaza kuwashikilia watu sita kwa tuhuma za kuharibu na kuiba nyaya za shaba katika mradi wa reli ya kisasa (SGR) maeneo ya wilaya za Mpwapwa na Bahi.

Vitendo hivyo vya kuiba miundombinu ya reli, ni wazi kama kweli watu hao wanahusika, basi watakuwa hawana uzalendo na nchi yao, wako tayari kufanya hujuma ili mradi huo usifanikiwe.

Ikumbukwe kuwa mradi wa SGR unajengwa kwa fedha nyingi, Watanzania wanatakiwa kuumbatia kwa manufaa yao na sio kufanya hujuma ambazo mwisho wake ni kusababisha ufe.

Sio kufa mradi tu bali pia hujuma zinaweza kuhatarisha maisha ya abiria wa treni hiyo ambayo imekuja kurahisisha usafiri wa kutoka na kuingia jijini Dar es Salaam kwa muda mfupi.

Tuwe wazalendo kwa miradi ya maendeleo ya nchi kwa kuweka mbele maslahi ya taifa, vinginevyo tunaweza kubaki tukilalamika kwamba nchi haina maendeleo na kumbe tunayakwamisha wenyewe.

Ni wajibu wa kila Mtanzania mzalendo kulinda miradi ya maendeleo katika eneo lake na kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika pale anapoona au kuhisi kuwapo vitendo vya hujuma.

Kila mmoja wetu akitambua hilo, hakutakuwa na hujuma kama hizo zilizoanza kujitokeza kwenye mradi wa treni iendayo haraka ambayo kwa sasa safari zake zinaanzia Dar es Salaam hadi Dodoma.

Binafsi ninaamini kuwa vitendo hivyo vinatokana na ukosefu wa uzalendo vinavyofanywa na baadhi ya watu wasiojali vitu vya umma wakidhani wao sio miongoni mwa umma wa Watanzania.

Labda nifafanue kidogo maana ya uzalendo, kwamba ni hali ya mtu kuipenda, kuithamini na kujitoa kwa ajili ya nchi yake. Mzalendo wa kweli daima anaweka maslahi ya nchi mbele na ya kwake binafsi nyuma.

kwa hiyo mzalendo ni mtu yeyote mzawa na mwenye kuipenda na kujitoa mhanga na saa nyingine ikibidi kufa kwa ajili ya nchi yake, lakini pia uzalendo unabeba dhana nyingi ukianzia asili, utamaduni, lugha, siasa, historia. Dhana zote zikifungwa kwenye dhana kuu ya utaifa.

Mtu anahujumu reli, bila kujali kwamba ndugu yake anaweza kusafiri kwa treni hiyo na kujikuta katika hatari zinazotokana na hujuma? Ninadhani wenye mawazo ya kufanya hujuma waachane nayo.

Waweke mbele uzalendo kwa kutanguliza utaifa mbele badala ya maslahi binafsi ambayo mwisho wake ni kusababisha madhara yanayotokana na hujuma zao wanazofanya katika miradi ya maendeleo.

Ugumu wa maisha usiwe kigezo cha kufanya hujuma ili kwenda kuuza\ vifaa vya reli, badala kila mmoja wetu anatakiwa kufanya kazi halali za kumwingizia kipato, sio kufanya wizi ukiwamo kama huo ambao watuhumiwa walikutwa na vifaa miundombinu ya treni ya SGR.

Hebu tuongozwe na sifa za uzalendo ambazo miongoni mwake ni kuona fahari kuzaliwa Tanzania, kuwa mwaminifu kwa kutoiibia nchi kwa njia yoyote na kutokuwa mharibifu wa mali na rasilimali za nchi.

# MAKALA

## FIKRA MBADALA

# Diaspora mliofanikiwa onekaneni, rudisheni



Pascal Mayalla

BADO niko nchini Marekani kwa ziara binafsi. Nimejitahidi kujichanganya na baadhi ya wanadiaspora wa Tanzania walioko nchini Marekani na kujiuliza wanafanya nini cha kueleweka na cha kuonekanika?

Nimejitahidi kuwasiliana na kile chama cha DICOTA lakini sikubahatika kupata ushirikiano mzuri lakini nitaendelea kuwatafuta wana diaspora wetu waliofanikiwa Marekani ili kujua wanafanya nini na hayo mafanikio yao, yanainufaisha vipi nchi yao?

Kupitia juhudi binafsi, nimefanikiwa kumwona dada mmoja wa Kitanzania aliyehamia Marekani mwaka 1999. Naomba nisimtaje jina kwa sababu sikumwambia kuwa nitaandika. Nimebaini kuwa diaspora wa Tanzania waliofanikiwa hapa Marekani, hawapendi kutajwa au kuandikwa wanafanya nini.

Huyu Dada ni mmiliki wa kampuni inayofanya biashara ya huduma na ameajiri zaidi ya watu 50, kila mwezi anawalipa mishahara ya zaidi ya Sh. milioni 500 za Kitanzania.

Kanikaribisha kwake, anakaa mtaa wa kitajiri, anamiliki nyumba kubwa ya ghorofa tatu na ana magari matano ya kifahari yakiwamo Benz ya G Wagon na gari la Kimarekani la Tesla linalotumia umeme. Kwa hesabu za haraka haraka, thamani ya magari hayo ni zaidi ya Sh. bilioni moja za Kitanzania.

Huu ni mfano mmoja tu wa Watanzania waliofanikiwa Marekani. Ametoa ajira kwa watu na kutengeneza faida kubwa. Nilipomwuliza kwanini asiwekeze Tanzania, alinijibu anasubiri uraia pacha ndipo afanye hivyo.

Imetokea mimi ninamfahamu huyu dada mpaka kwao, Sanya Juu, wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro ambako nimefika. Kabla sijaja Marekani, nilipita kwao na hali niliyoiona ya umasikini wa hapo kijijini kwao, nikilinganisha na maisha ya kitajiri na kifahari anayoishi Marekani, ni mbingu na nchi!

Huu ni wito kwa serikali yetu kuharakisha mkakati wa uraia pacha ili diaspora wa Tanzania waliofanikiwa ughaibuni, waje kuwekeza nyumbani na kurudisha shukrani nyumbani.

Mtu Mtanzania ana magari matano ya kifahari Marekani, anaendesha kwa kubadilisha tu, halafu ile hospitali ya Kibon'goto pale Sanya Juu, kuna wajawazito, wanajifungulia chini kwa kukosa kitanda. Ile G-Wagon moja tu ingejaza vitanda hospitali nzima au madawati shule nzima.

Nimetembelea maeneo mbalimbali ya Marekani kudhani labda ningeona mafanikio ya kuonekanika ya diaspora wa Tanzania, zaidi ya huyu dada kunikaribisha kwake. Sikufanikiwa kuona kitegauchumi chochote cha Mtanzania. Kila rais wetu akija Marekani ni kukutana na Watanzania waishio Marekani na kubadilisha mawazo tu. Rais wa Kenya akija Marekani anafungua miradi ya diaspora wa Kenya.

Muda aliokuja Marekani huyu dada wa Tanzania, ni mwaka 1999. Ni muda huo Mkenya Kevin Onyona, alihamia Marekani na kuajiriwa na Home Depot, kampuni ya kimataifa ya uboreshaji wa nyumba Marekani.

Sasa hivi ni mmiliki wa migahawa ya Swahili Village ambayo ni miongoni mwa migahawa bora zaidi ya vyakula vya Kiafrika nchini Marekani. Kevin Onyona alianzisha mlolongo wa migahawa hiyo mwaka 2016 na leo inajivunia migahawa mitatu. Miaka sita baadaye, alitumia migahawa yake kujenga uhusiano halisi kati ya utamaduni wa Kiafrika na dunia nzima.

Mkahawa mkuu wa Swahili Village unapatikana Rhode Island Ave, Beltsville na mingine mingine miwili iko Washington DC na New Jersey. Mgahawa wa Washington DC ulifunguliwa na aliyekuwa Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta.

Wito kwa diaspora wetu, najua kuna uwezekano kuna mambo makubwa mazuri ya kuonekana kwa diaspora wa Tanzania wanafanya. Natoa wito kwa Diaspora wetu, anekanikeni basi.

Mimi Pascal Mayalla, mwandishi wa habari na mtangazaji wa kujitegemea, ninayeandaa vipindi vya TV, redio, makala magazetini na kwenye mitandao ya kijamii, nikifanya kazi kupitia kampuni ya PPR, www.ppr.co.tz, nimetua rasmi nchini Marekani kwa ajili ya kufungua ofisi.

**KIPINDI KIPYA**

TAK ni kipindi kipya cha TV chenye lengo la kuiangazia Tanzania kitaifa, kikanda na kimataifa kuhusu mambo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ambayo yanaihusu Tanzania kwenye medani za kimataifa. Kipindi hiki kitaimulika Tanzania kwenye mikutano ya kimataifa, ukiwamo mchango wa diaspora wa Tanzania na wakati huo huo kuangazia fursa mbalimbali za kimataifa kwa Watanzania kuzichangamkia.

Kipindi hiki kitarushwa kwenye local channels za TV za Tanzania, DSTV, Star Times na kwenye online media.

Nikiwa Mtanzania mzalendo, ninaumia sana kila ninapoona diaspora wa wenzetu wanafanya mambo makubwa yanayoonekana na kujiuliza diaspora wetu wanafanya nini? Mbona hatuwaoni?. Kwa hiyo napenda kuona Tanzania tunafaidika na mchango wa wana diaspora wetu kwa kiwango cha juu huko walipo, kuitumia kulisaidia taifa letu kisiasa, kiuchumi cha kijamii.

***Paskali***

## KONA YA AFYA

# Namna ya kutambua, kuzuia mshtuko wa moyo



Na Dk. Mabula Budodi

NAIKUMBUKA hiyo siku naiona kama jana tu. Hakika sitaisahau kabisa. Ilikuwa siku mbaya zaidi kuwahi kutokea maishani mwangu. Ni siku ambayo nilitambua kwamba ni jambo rahisi sana kupoteza maisha kwa mwanadamu," alisikika mwathirika wa mshituko wa moyo akieleza.

Anasema ilikuwa asubuhi ya machweo jua likichomoza akiwa amemaliza kujiandaa na kutaka kwenda kazini. Alianza kusikia maumivu ya kifua yaliyoanza ghafla huku yakiongezeka kuwa makali ndani ya muda mfupi.

"Maumivu hayo yalinzia upande wa kushoto wa kifua kwenda shingoni hadi mkono wa kushoto. Upande wote ulipata ganzi na maumivu yalikuwa makali. Hali hiyo ilifatiwa na kuhisi maumivu ya kichwa, upungufu wa pumzi, kichefuchefu, kutokwa jasho na kizunguzungu.

"Nilipelekwa hospitali ya karibu na mke wangu. Madakitari walinipokea kwa haraka katika kitengo cha dharura na kunipa dawa za maumivu na kuanza kufanya vipimo vya damu na moyo muda huo huo.

"Daktari alisema kwa namna ya maumivu unayoyapata, unaweza kuwa umepata mshituko wa moyo. Aliomba nifanyiwe kipimo cha moyo ambacho aliniambia ni kwa ajili ya kupima umeme wa moyo kuangalia ufanyaji kazi. Nilifanyiwa kipimo hicho huku nikiwa na hofu kubwa sana huku maumivu yakiwa yamepata hauweni kwa kiasi," anabainisha.

Anasema aliwekewa nyana nyingi kifuani, mikononi na miguuni huku akiambiwa ajaribu kutulia kidogo ili kupata kipimo kizuri zaidi na akafanya hivyo. Picha ya kipimo cha moyo ilipotoka, daktari alisema angechelewa kidogo angeweza kupoteza Maisha.

Kwa mujibu wa mtu huyo, daktari aliemweleza kuwa alikuwa amepata mshituko wa moyo kwa maana kwamba sehemu ya moyo haipati damu vizuri hali ambayo husababisha misuli ya moyo kuumia na kuharibika. Anasema daktari huyo alisema kama angechelewa zaidi, sehemu kubwa ya moyo ingekufa na kushindwa kufanya kazi.

Baada ya kumweleza hayo, anasema alimpa rufaa ya kwenda kwa ajili ya matibabu zaidi katika ilibidi wamhamishie Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kitengo cha dharura kwa ajili ya matibabu zaidi. Waliwasiliana na madakitari wa JKCI na kuagoza wamwahishe na walipofika walikuwa wameshajiandaa na kuanza matibabu moja kwa moja.

"Nilipofika nilikuta madaktari bingwa wa moyo wakiwa wanasubiri nje kwa ajili ya kunipokea kutoka kwenye ambulansi. Walinipokea, walinipima tena na kuanza matibabu ya moyo mpaka nilivyopata nafuu.

"Madakitari waliniambia hakika una bahati sana maana watu wengi huwa wanagundulika kwa kuchelewa, vivyo kufikishwa tatizo likiwa limeshakuwa kubwa zaidi," anasimuliza zaidi.

Baada ya matibabu na kupata hauweni, anasema madaktari walitumia muda mwingi kuanza kufatilia jambo gani lilisababisha kupata tatizo hilo licha ya kwamba awali hakuwa na shinikizo la damu wala sukari.

Hata hivyo anakiri kwamba zamani alikuwa anavuta sigara sana kwa kumaliza hata paketi mbili kwa siku na alikuwa na uzito mkubwa, vitu ambavyo madaktari waqlimwambia kuwa vinaweza kuwa vimechangia kupata tatizo hilo. Pia ilionekana mafuta ya lehemu kwenye damu, hivyo kuwa sababu nyingine iliyochangia kupata mshituko wa moyo.

Baada ya kugundua hivyo, anasema walimwanzishia dawa na kliniki ya moyo ambayo hadi sasa anahudhuria na anaendeea vizuri.

Mshituko wa moyo ni hali ya hatari inayotokea kwenye moyo kwa sababu ya moyo kukosa okisijeni baada ya mishipa midogo inayopeleka damu kwenye moyo wenyewe kuziba kabisa au kiasi. Hali hiyo husababisha sehemu ya moyo iliyokosa damu kuharibika na kushindwa kufanya kazi yake sawia.

**DALILI ZAKE**

Dalili za mshituko wa moyo ni maumivu ya kifua ya kati au kushoto upande wa moyo yanayobana kifua. Maumivu haya huweza kuelekea shingoni, mgongoni au mkononi kama ganzi, upungufu wa hewa, yaani kuhisi kushindwa kupumua bila kuwa na maumivu ya kifua, kutokwa jasho, kizunguzungu, kichwa kuuma kwa mbali kama mtu anapata mawenge, kichefuchefu au kiungulia.

**WALIO HATARINI**

Watu wenye shinikizo la damu wako kwenye hatari ya kukumbwa na tatizo hilo. Shinikizo la damu huchangia kuharibu mishipa ya damu, hivyo kuifanya kuwa rahisi zaidi kuziba.

Sababu nyingine ni ongezeko la lehemu mwilini, yaani mafuta yanayoganda kwenye mishipa ya damu baada za kuongezeka maradufu kupita kiasi, hivyo kuziba mishipa ya damu.

Ugonjwa wa sukari kwa kiasi kikubwa huongeza madhara yanayotokea kwenye moyo, hivyo ni vyema kutumia dawa za sukari na kufatilia afya vizuri.

Unene uliopitiliza unaweza kusababisha kupata kisukari, shinikizo la damu na hata kuwa na lehemu nyingi ambayo huchangia kwa kiasi kikubwa kupata mshituko wa moyo.

Uvutaji wa sigara huchangia kuharibu mishipa ya damu pia kuchelewa kupona kwa mishipa pale inapoharibika kwa sababu ya nikotini inayopatikana kwenye tumbaku ya sigara.

Kula chakula chenye mafuta mengi, yaani kupendelea vyakula vya kukaanga huchangia kuongeza mafuta mwilini maradufu. Pia kutokufanya mazoezi huchangia koungeza mafuta mwilini na mwishowe kutuzwa kwenye mishipa ya damu.

**NAMNA YA KUZUIA**

Kuzuia au kupunguza uwezekano wa kupata mshituko wa moyo, huhusisha kufanya mazoezi angalau dakika 150 kwa wiki, kutokuvuta sigara, kula vizuri vyakula kama mboga, matunda na mbegu, kupunguza msongo wa mawazo, kudhibiti magonjwa ya kisukari na shinikizo la damu.

Jambo la muhimu la kuzingatia ni kuangalia afya mara kwa mara kwa wataalamu wa afya na kupata ushauri wa dakitari.

***•Dk. Budodi ni daktari wa binadamu anapatikana kwa namba 0710 980096 na barua pepe mabulabudodi@gmail.com***

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Kijaji asisitiza matumizi nishati safi ya kupikia

**Na Mwandishi Wetu,** BAKU, AZERBALIAN

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji, amehimiza mataifa yaliyoendelea kuunga mkono juhudi za nchi zinazoendelea ili kutekeleza kikamilifu ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Dk. Kijaji alitoa wito huo juzi kwenye Mkutano wa Viongozi wa Masuala ya Nishati Safi ya Kupikia uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) unaofanyika mjini hapa.

Alisema mkutano huo ni sehemu ya mkakati wa kuunga mkono juhudi za kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kuondokana na matumizi ya nishati chafu.

Katika mkutano huo, Kijaji aliambatana na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Jackson Kiswaga, pamoja na Mshauri wa Rais wa katika masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Dk. Richard Muyungi.

Waziri Dk. Kijaji pi alikutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi wa Kampuni ya Burn Manufacturing, Caroline Amollo. Kampuni hiyo inajihusisha na utengenezaji wa majiko ya nishati safi ya kupikia nchini Tanzania.

Katika mazungumzo yao, Waziri Kijaji aliishukuru na kuipongeza kampuni hiyo kwa uwekezaji kwenye nishati safi ya kupikia ambayo ni agenda namba moja ya Rais wa Dk. Samia Suluhu Hassan.

Pia amemhakikishia Amollo kuwa serikali ya Tanzania itaendelea kuipa ushirikiano kampuni hiyo ili kusaidia katika upatikakanaji wa nishati safi ya kupikia nchini.

Amollo kwa upande wake, aliishukuru Tanzania na kuahidi kuwekeza zaidi kwenye nishati safi ya kupikia ili kuhakikisha inapatikana kwa wingi na kwa bei nafuu.

Katika hatua nyingine, Waziri Kijaji alikutana na kufanya mazungumzo na Rais na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Tomorrow, Rei Goffer. Kampuni hiyo inajishughulisha na masuala ya teknolojia ambayo inasaidia kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi katika sekta za usafirishaji, mawasiliano, kilimo na uvuvi.

Katika mazungumzo hayo, Dk. kijaji aliyeambatana na wataalam kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), aliikaribisha kampuni hiyo kuwekeza nchini na kuahidi kuwa Tanzania itatoa ushirikiano ambao itahitaji ili kuhakikisha inanufaika na miradi ya Tomorrow.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Ashatu Kijaji (katikati), akizungumza na Mkurugenzi wa Kampuni inayojihusisha na utengenezaji wa majiko ya nishati safi ya kupikia nchini Tanzania ya Burn Manufacturing, Caroline Amollo, katika mkutano uliofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) mjini Baku, nchini Azerbaijan, juzi. Kulia ni Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Cyprian Luhemeja. **PICHA: OMR**

# Tanzania, Uganda zakubaliana uimarisha mpaka wa kimataifa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameitaka familia iliyofiwa na vijana wawili hivi karibuni Tazari, Kaskazini A Unguja, kuwa na subira.

Amesema kutokana vifo hivyo, serikali ina wajibu wa kutafuta ukweli kuhusu tukio hilo.

Othman aliyasema hayo juzi alipowasalimia wananchi alipofika kijijini hapo kutoa mkono wa pole kwa familia iliyopoteza vijana wao wiki iliyopita katika mazingira ya utatanishi.

Alisema linapotokea jambo kama hilo kwa yeyote aliyehusika ni wajibu wa serikali kuutafuta ukweli na kuuweka hadharani bila kuficha ili jamii ifahamu kile kilichotokea.

Pia alisema njia hiyo ni muhimu katika kusaidia na kuzuia matukio ya namna hiyo kujirudia na kwamba pia inasaidia kupatikana ukweli na sababu zililozofanya kutokea jambo kama hilo na haki kutendeka.

Alisema bila serikali kutafuta ukweli halisi na kufahamika, ni vigumu kutatua tatizo lililosababisha hali hiyo na kudhibiti kujirudia kwa hali hiyo.

Othman aliwapongeza wananchi hao kwa ustahamilivu kwenye jambo hilo licha ya kuwapo changamoto kubwa iliyojitokeza na kwamba itasaidia kuweka jitihada na serikali kutimiza wajibu wake kudibiti matatizo kama hayo. Aliwaahidi wananchi hao kwamba serikali itahakikisha kila mwenye haki kwenye jambo hilo atapata na kuwasihi wananchi kuendelea kuwa watulivu kama walivyoonesha wakati tukio hilo la vifo lilipotokea.

Awali, wanafamilia wa vijana hao walimweleza Othman kwamba pamoja na suala hilo la msiba kutokea katika hali hiyo ya kutatanisha, kuna haki za msingi za marehemu, hivyo ni vyema zikafanyiwa utaratibu kupatikana. Walisema hawajapata ushirikiano wa polisi kuhusu jambo hilo licha ya kufuatilia.

Makamu wa Kwanza wa Rais alifika katika kijiji cha Fukuchani kutoa mkono wa pole na kushiriki katika hitima ya kumwombea dua Mwenyekiti wa Jimbo la Nungwi wa Chama cha ACT Muhamad, Ali Muhamad, aliyefariki dunia mapema wiki hii na kuzikwa kijijini hapo.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini A Unguja, Othman Ali Maulid, akimkaribisha Othman, aliwapa pole wanafamilia na kuwataka kuwa na subira kwa vile kifo ni njia ya wote.

# MUHAS yatoa nyaraka vita ukatili wa kijinsia

**Na Grace Mwakalinga**

CHUO Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS),kimetengeneza miongozo miwili ya jinsia, ikiwamo wa sera ya kuzuia na kupambana na unyanyasaji wa kijinsia pamoja na sera ya ujumuishi.

Miongozo hiyo imeidhinishwa na Baraza la Chuo hicho kwa ajili ya kutumika kutoa huduma za elimu zinazozingatia masuala ya kijinsia.

Naibu Mratibu wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Uchumi (HEET), Dk. Nathanael Sirili, alisema hayo jana wakati wa hafla ya kutia saini mkataba wa ujenzi wa Ndaki ya Tiba kati ya MUHAS na makandarasi wa mradi huo, Mohammed Builders na Hainan International Limited, iliyofanyika Mloganzila, Dar es Salaam.

Dk. Sirili alisema miongozo hiyo ni miongoni mwa masuala yanayotekelezwa na chuo kupitia mradi wa HEET, ulioanza kutekelezwa mwaka 2021 hadi 2026.

Pia alisema MUHAS imehuisha mitaala 82 na kuboresha mbinu za kufundishia kwenye ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu kwa kufanya mapitio na tayari mitaala 23 ya programu imeandaliwa.

Alisema kuwa madhumuni ya maboresho hayo ya mitaala ni kuhakikisha inaendana na mabadiliko ya tabianchi, soko la ajira, mabadiliko ya magonjwa, teknolojia pamoja na kuzingatia mahitaji ya makundi mablimbali yaliyopo katika jamii.

"Mitaala 73 tayari imeshapata Ithibati kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) huku 32 iliyobaki ikiendelea kupitiwa na tume na kuboreshwa," alisema Dk. Sirili.

Mratibu wa HEET chuoni hapo, Prof. Erasto Mbughi, alisema Sh. bilioni 50 zitatumika kujenga miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Kampasi ya Mloganzila na Kigoma.

Alisema katika fedha hizo, Mohammed Builders itatumia Sh. bilioni 23.5 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala ndani ya tiba, maktaba na TEHAMA, uwanja wa mpira wa miguu na barabara ya kuingia kwenye majengo husika.

Kampuni ya Hainan International Limited itatumia Sh. bilioni 26 kujenga kumbi za mihadhara, maabara za kufundishia, jengo la Anatomia, mabweni ya wanafunzi na bwalo la chakula.

Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa Apolinary Kamuhabwa, alisema ni miongoni mwa wanufaika wa mradi wa HEET ambapo kwa kampasi ya Mloganzila na Kigoma kupitia mkopo wa Benki ya Dunia walitengewa kiasi cha Sh. bilioni 113 .

Alisema mbali na fedha hizo kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia pia wataendeleza wahadhiri kitaaluma katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kuboresha mifumo ya Teknolojia na Mawasiliano (TEHAMA) ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli za kitaaluma.

# MAISHA

NOVEMBA 17, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 12

## FUNGATE



Ukurasa 13

## Fulana ya kupumua suluhisho majira ya joto



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Andaa nyumba ya kijijini kwenu




# Njia ya kuzuia fangasi za kucha

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | 3 | 2 | 1 |
| 2 | 1 | 4 | 3 |
| 1 | 2 | 3 | 4 |
| 3 | 4 | 1 | 2 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M | ■ | M | B | O | G | A |
| A | ■ | ■ | ■ | G | ■ | M |
| K | ■ | F | U | O | ■ | I |
| O | G | O | ■ | P | E | N |
| N | ■ | N | O | A | ■ | I |
| D | ■ | Z | ■ | ■ | ■ | K |
| E | K | A | N | A | ■ | A |


## FUMBO TOTO



Jaza majina ya nchi ambazo miji yake imetajwa hapa chini.

LIBREVILLE, MUSCAT, ACCRA, LUANDA, TOKYO, TAIPEI

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

HAYA WADOGO ZANGU, TUENDELEE NA AMSHA AKILI IITWAYO SUDOKU. JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | | | 4 |
| | 2 | | 1 |
| | | | |
| 3 | 1 | | |

## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MAMA mmoja alikuwa anafanya usafi chumbani na ghafla aliona madaftari yakiwa yamehifadhiwa uvunguni mwa kitanda cha mtoto wake.

Haraka alimfuata motto wake wa kumuuliza kwa hasira

**Mama:** Mwanangu haya madaftari ya nini?

**Mtoto:** Madaftari ya Hisabati

**Mama:** ya nani?

**Mtoto:** yale uliokuwa ukininunulia, nilikuwa nayahifadhi humo kwa sababu somo la hisabati siliwezi

**Mama:** Nitamwambia mwalimu wako akupe adhabu.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Shuhuda ndoto zinavyotesa na kuua watu

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na uchambuzi wetu juu ya ndoto unazoota usiku. Tayari tumeangalia maana ya ndoto na aina zake. Pia sababu za kuota ndoto unazoziota.***

Leo tuende zaidi kuona shuhuda jinsi shetani anavyoshambulia watu kupitia ndoto. Hebu sikia shuhuda hizi upate picha mashambulizi yanavyofanyika ukiwa umelala, kisha inakuwa uhalisia.

Watu wengi wamefungwa kutokana na kushambuliwa kwenye ndoto. Mbegu nyingi za uharibifu kwenye maisha ya watu wengi zimepandwa kupitia ndoto. Matatizo ya maisha ya watu wengi leo yametokana na kushambuliwa kwenye ndoto.

Magonjwa mengi yasiyo na tiba hospitalini chanzo chake ni mbegu za kichawi zinazopandwa na shetani kupitia ndoto. Neno la Mungu linasema, "lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake"(Mathayo 13:25).

Wengi wameunganishwa na nguvu za kichawi, pia nguvu za kuzimu kupitia ndoto. Hebu sikia shuhuda hizi kupata picha ya kile ninachozungumzia hapa.

Nilisikia ushuhuda wa dada mmoja aliyekuwa na umri miaka 43 aliyekuwa akitafuta mume wa kumuoa bila mafanikio. Wadogo zake wote walikuwa wameolewa na wana miji yao isipokuwa yeye.

Mbali na yeye kuwa na umri mkubwa bila kuolewa ijapokuwa alikuwa na sifa zote za kuolewa, ilimlazimu atafute msaada wa kiroho. Baada ya maombi makali ya kufichua, ilisikika sauti ikisema, "muulize akiwa na umri wa miaka 16 aliota nini? Wewe muulize, mimi ni mume wake. Hawezi kuolewa na mwanaume yoyote isipokuwa mimi!"

Alipozinduka baada ya kuombewa na kuulizwa kwa habari ya hiyo ndoto, alikumbuka na kusema, nikiwa na umri wa miaka 16 niliota nipo kwenye sherehe nyumbani kwetu.

Wakati tunaburudika na muziki, ghafla lilitokea jitu kubwa likiwa linasema, "mimi ni mume wako, sitakubali uchukuliwe na mtu mwingine".

Alipozinduka kutoka usingizini alipuuzia hiyo ndoto kama ilivyo kawaida ya watu wengi pasipo kujua kuwa tayari alikuwa amefungwa na hilo jitu kupitia ndoto. Baada ya maombvi dada huyu alifunguliwa na kupata mume aliyefunga naye ndoa takatifu kanisani.

Maandiko ya Mungu yanasema shetani ni mwizi na kazi yake ni kuiba, kuchinja na kuharibu(Yohana 10:10); na kwa sababu hiyo yupo tayari kuhakikisha anatumia mbinu yoyote ile ili tu aharibu maisha ya mwanadamu. Shetani anaweza kutumia ndoto kuwatisha na kuwafunga wanadamu. "Hapo nisemapo, kitanda changu kitanitunza moyo, malazi yangu yatanipunguzia kuugua kwangu, ndipo unitishapo kwa ndoto na kunitia hofu kwa maono.(Ayubu 7:13-14).

Msomaji wangu, hebu sikia tena ushuhuda huu. Mama mmoja aliota ndoto ya ajabu na kutisha, iliyokatisha maisha yake. Aliota anayonyesha mtoto. Cha kushangaza mtoto huyo alikuwa na sura mbaya ya kutisha. Alipojaribu kumtoa kifuani, yule mtoto aling'ata chuchu za maziwa yake na kusababishia majeraha!

Aliposhtuka kutoka usingizini alishangaa kuona vidonda kwenye matiti yake na alikuwa akihisi maumivu makali sana. Baada ya siku mbili matiti yalianza kuvimba. Alipokwenda kupima hospitali iligundulika kuwa ni kansa yaani saratani ya matiti. Baada ya wiki mbili alifariki dunia!

Mpenzi msomaji wangu. Bila shaka umepata picha kuhusu ndoto na madhara yake. Yapo maswali unapaswa kujiuliza baada ya kuota ndoto. Je, hii ndoto ni ya Mungu? Je, ndoto hii ni Roho Mtakatifu anathibitisha kitu?

Au je, ndoto hii inainua au inashusha? Je, hii ndoto inajenga au inabomoa. Je, hii ndoto inaashiria vifungo kwenye maisha yangu? Je, hii ndoto inaogofya? Je, hii ndoto inaleta amani au hofu?

Je, mwisho wa ndoto ni mzuri au mbaya? Je, hii ndoto inanionya au inanitahadharisha? Je, hii ndoto inanifariji? Au hii ndoto inanifundisha? Yapo maswali mengi unapaswa kujiuliza kuhusiana na ndoto unazoziota.

Kumbuka, Mungu hutumia ndoto kumrekebisha mtu. Alifanya hivyo kwa Yusufu mwana wa Yakobo. Ndoto yaweza kukuonya na kukuepusha na jambo fulani au hatari iliyoko mbele yako. Wengi leo wanajuta, kisa walipuuzia ndoto walizoota.

Ndoto ni siri, ni baraka. Kwenye ndoto unaweza kupandikizwa roho ya Herode inayoua vitu vichanga. Ukianzisha biashara inakufa, huduma katika kazi/ajira na kadhalika. Unapoanzisha vitu weka ulinzi visiuawe na maadui.

***Wiki ijayo: Baadhi ya aina za ndoto na madhara ya ndoto mbaya. Ujumbe 0715268581, ipo WhatsApp.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Nani wa kuviamsha vijiji kuchangamkia Uchumi?

JUMUIYA ya Hifadhi za Wanyamapori (WMA), ni eneo kwenye ardhi ya kijiji au vijiji iliyokubalika na kutengwa kwa misingi ya kuhifadhi wanyamapori na kwa ajili ya biashara inayotokana na uhifadhi katika taifa.

Usimamizi wa shughuli za jumuiya hizi, kisheria unaratibiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA).

Katika maeneo yanayopakana na hifadhi za taifa, serikali imeruhusu jamii kuanzisha hifadhi za wanyamapori, hususan kwenye maeneo yanayozunguka hifadhi za taifa au hifadhi zingine.

Ruhusa hiyo pia, inatoa fursa ya kuanzishwa jumuiya hizo kwenye ushoroba (njia maalum za wanyama), ambapo wanyama wanasafiri kutoka hifadhi moja kwenda nyingine kwa ajili ya kutafuta chakula, maji na mahitaji mengineyo. Ni muhimu kukumbuka kuwa WMA si Hifadhi ya Taifa na wala si mwendelezo wa Hifadhi za Taifa au ardhi inayomilikiwa na mtu binafsi. Vijiji vinaweza kutoa leseni kwa wawekezaji binafsi ili kujenga miundombinu au kuendesha shughuli zao ndani ya maeneo ya WMA, mfano kujenga kambi na kuendesha uwindaji.

Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998, inabainisha kuwa jamii itakuwa na mamlaka yote ya kusimamia na kupata manufaa kutokana na juhudi zao za uhifadhi, ingawa umiliki wa rasilimali za wanyamapori unabaki kwa serikali. Hata hivyo, Kanuni za WMA za Mwaka 2018 zinaeleza kuwa mgawanyo wa manufaa utaelezwa na waraka utakaokuwa ukitolewa mara kwa mara', ambao ni waraka wa mwaka 2020,

Waraka huo pamoja na mambo mengine, unaeleza kuwa mapato yatokanayo na shughuli za uhifadhi yaende moja kwa moja kwa Serikali, ambayo itarudisha sehemu ya mapato hayo kwenye WMA. Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu shughuli za kamati hiyo kwa mwaka 2023, iliyowasilisha Bungeni na Mwenyekiti wake, Timotheo Mnzava, mchanganuo wa mgawanyo wa mapato yatokanayo na shughuli za uwindaji wa kitalii kwenye WMA uko hivi.

Kwenye chanzo cha mapato ambayo ni ada ya kitalu, TAWA inanufaika na asilimia 25, WMA asilimia 75, wakati katika ada ya uwindaji, TAWA inachukua asilimia 25, WMA asilimia 55, halmashauri husika inanufaika kwa asilimia 10 na asilimia 10 inakwenda Hazina (Mfuko Mkuu wa Serikali).

Aidha katika ada ya uhifadhi, TAWA inapata asilimia 25, WMA inachota asilimia 45, Halmashauri inaambulia asilimia tano na Hazina asilimia 25.

Vilevile, suala la ada ya watazamaji TAWA inanufaika kwa kupata asilimia 25, WMA asilimia 60, Halmashauri ya Wilaya asilimia tano na Hazina, asilimia 10.

Wakati ada inayotokana na kibali, TAWA inapata asilimia 25, WMA inanufaika asilimia 30, Halmashauri inapata asilimia tano na Hazina inachukua asilimia 40.

Akieleza changamoto zinazozikabili jumuiya hizo kwa sasa, Mnzava ambaye pia ni Mbunge wa Korogwe Vijijini, anasema katika uchambuzi wao kwenye eneo hilo, Anasema wamebaini kuwa baada ya serikali kuanzisha mfumo wa kupeleka moja kwa moja katika mfuko mkuu, mapato ya taasisi mbalimbali, ikiwemo taasisi za uhifadhi, mapato yatokanayo za WMA nayo yamekuwa yakiingia moja kwa moja katika mfuko mkuu wa serikali.

Anasema hali hiyo inazorotesha shughuli za uhifadhi katika maeneo hayo kwani, jumuiya hizo huingia gharama katika uhifhadhi wa maeneo hayo.

Sasa, anasema kwa kuwa WMA zinafanya kazi kubwa katika uhifadhi kwa kudhibiti ujangili wa wanyamapori na kutatua changamoto ya muingiliano wa binadamu na wanyama wakali na waharibifu; Na kwa kuwa, utekelezaji wa jukumu hilo unahitaji fedha ambazo zinatokana shughuli zinazofanywa katika WMA ambazo hukusanywa moja kwa moja na serikali, na serikali imekuwa ikichelewesha kurejesha fedha hizo kwenye WMA.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, serikali ihakikishe inarejesha kiasi chote cha fedha kinachostahili kurejeshwa kwenye WMA kwa mujibu wa kanuni ili kuziwezesha katika kuendesha na kuratibu shughuli zao kwa ufanisi.

Lakini pia serikali iandae mpango wa ukusanyaji wa mapato ambao utatofautisha mapato ya Serikali na yale ya WMA ili fedha za jumuiya hizi ziende moja kwa moja kwenye akaunti zao.

Kadhalika, serikali ishughulikie na kutatua migogoro ya mipaka kati ya maeneo ya hifadhi na WMA mbalimbali nchini.

Swali unaloweza kujiuliza ni je, wananchi wanaweza je kunufaika na uhifadhi?

Wizara ya Maliasili na Utalii, inaendelea na juhudi za kuhakikisha wananchi wanaoishi jirani na maeneo ya hifadhi, wananufaika na rasilimali zilizopo?

Kupitia Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori, jamii zinanufaika kwa kupata ajira, kitoweo, elimu, miradi ya kijamii na kuongeza kipato. Aidha, wananchi wanaoishi jirani na misitu wananufaika kupitia miradi ya ufugaji nyuki ambapo kupitia uwezeshaji wa Mfuko wa Misitu Tanzania,

Iko miradi mingi imeanzishwa kwa ajili ya kuboresha kipato cha jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu imetekelezwa. Faida nyingine ni udhibiti wa migogoro baina ya wananchi na hifadhi. Katika kudhibiti migogoro ya mipaka kati ya wananchi na maeneo jirani na hifadhi, jumuiya nyingi za uhifadhi za kijamii zimeanzishwa.

Tanzania imetajwa kuwa miongoni mwa nchi chache barani Afrika ambazo zinatekeleza dhana ya ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa kivitendo kwa kutoa fursa kwa wananchi kushiriki moja kwa moja katika kusimamia rasilimali za wanyamapori.

WMA nchini zinachukuliwa kama ni kinga (buffer) muhimu kwa maeneo ya Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Hifadhi ya Ngorongoro na Mapori Tengefu.

Yote hiyo ni kwa sababu bila WMA, changamoto za kiuhifadhi, zitaathiri moja kwa moja Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Hifadhi ya Ngorongoro na Mapori Tengefu. Kutokana na faida na umuhimu wake kiuchumi kwa jamii zinazozunguka maeneo yanayoruhusu jamii kunufaika na fursa hiyo, ni vyema wadau wa uhifadhi nchini wakaendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kuendeleza WMAs ili kuziwezesha kujisimamia na kujiendesha.

Pamoja na hayo, kupitia ushirikishwaji huo, jamii zitakuwa zikinufaika na matunda yatokanayo na shughuli za uhifadhi katika maeneo yao kwa kujiletea maendeleo na huduma za kijamii ikiwamo shule na zahanati.

***• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# FUNGATE







Wakiwa na sura za furaha katika kutimiza ndoto zao, John na Frida walikuwa katika siku isiyosahaulika katika visiwa vya Zanzibar hivi karibuni. PICHA: MC GaraB







# MITINDO










## Fulana za kupumua suluhisho majira ya joto

MAJIRA ya joto yamewadia, watu wanatakiwa kuvaa nguo nyepesi na zenye uwezo wa kuufanya mwili kupumua.

Katika kipindi hiki joto huwa kali, mwili unapambana na hali ya hewa kwa kutoa jasho, hivyo ni muhimu kuvaa nguo zinatoa uhuru wa kufanya shughuli zako mbalimbali bila kuathirika.

Na hapo ndipo fulana za kupumua za majira zinapendekezwa kuvaliwa na kuwa mwokozi sahihi katika kudumisha hali ya utulivu wa mwili.

Fulana hizi zenye matundu ya kupumua ni nzuri kuvaliwa kwa kuwa imetengeneza na vitambaa vyepesi na laini.

Kiuhalisia, fulana za aina hii zina umbo linalovutia, ubora wa kitambaa na mikato yenye mitindo ya kipekee inayopendeza kwa kila mtu.

### VIGEZO MUHIMU

Unaponunua fulana za kupumua lazima ujihakikishie kama ina vigezo muhimu kama ukubwa wa matundu ya kupumua au malighafi iliyotengenezewa vina kaboni inayoruhusu ngozi yako kupumua.

Pia angalia kama ina nyuzi nyepesi kwa mtiririko wa kutoa hewa juu, uwezo wa kunyonya unyevu na kukufanya uwe mkavu.

## UREMBO

Na Mary Geofrey



# Njia kuzuia fangasi za kucha

KILA eneo la mwili lipo hatarini kushambuliwa na kiwango fulani cha fangasi, iwe kwenye kucha, ngozi, mdomoni na sehemu za siri.

Unaanza kuugua fangasi pale vimelea hao wanapomea kupita kiasi. Vimelea wa fangasi wakua zaidi kwenye mazingira ya unyevunyevu na joto.

Vimelea wa fangasi waliopo ndani ya mwili wako wanaweza kukuletea athari pale mazingira ya mwili yanapovurugika.

Pia endapo utagusana na mtu mwenye maambukizi unaweza kupata fangasi.

Wale ambao wapo hatarini kupata tatizo la fangasi za kucha ni wale wanaovaa viatu muda mrefu, wanaobandika kucha na wenye majeraha ya kucha.

### DALILI

Fangasi kwenye kucha moja inaweza kuathiri pia kucha ya kwenye kidole kingine na pia hata kidole chenyewe. Dalili kubwa ni pamoja na kupinda kwa kucha, harufu mbaya kutoka kwenye kucha na kucha kuwa ngumu sana na nene.

### NJIA ZA KUTIBU

Si salama kujinunulia dawa na kutumia pasipo kumuona daktari. Daktari anaweza kupendekeza dawa mbalimbali za kumeza ili kupambana na fangasi.

### NJIA ZA KUZUIA

Osha mikono yako baada ya kushika kucha iliyoathirika, kausha vidole vizuri baada ya kuoga hasa katikati ya vidole vya miguu na pata huduma za 'manicure' na 'pedicure' kutoka kwenye saluni ya kuaminika.

Epuka kutembea peku kwenye maeneo ya watu wengi na punguza matumizi ya kucha za bandia na rangi za kupaka kucha.

## MAPISHI

# Maharage ya kukaanga

MBOGA ya maharage ni maarufu hapa kwetu Tanzania ambayo inaliwa na familia karibu zote.

Mboga hii kuna namna nyingi za kuiunga kwa nazi na mafuta na kitunguu kwa kuunga moja kwa moja, lakini leo tuna pishi lingine la kukaanga.

### Mahitaji

Maharage robo kilo, tui jepesi kikombe kikubwa kimoja, tui zito robo jagi, kitunguu thomu kilo twangwa kijiko cha chai kimoja kitunguu maji kilochokatwa, pilipili hoho iliyokatwa 1, keroti na chumvi kijiko kimoja cha chakula.



Mafuta ya kula vijiko viwili, royco kijiko kimoja cha chakula , nyanya zilizosagwa tatu na maji ya kuchemshia kiasi.

### Jinsi ya kupika

Funika sufuria kisha chemsha maharage mpaka maji yapungue, ongeza maji mengine yaache yachemke mpaka yapungue na sasa weka maji kidogo kidogo yasifunike maharage yako ili yaive bila ya kutoka magamba.

Endelea kuongeza maji kidogo kidogo mpaka yaive, weka mafuta kwenye sufuria nyingine na acha yapate moto.

Weka vitunguu maji vikaange hakikisha haviungui, ongeza pilipili mboga na ikaange vizuri, weka keroti endelea kukaanga na mwisho weka kitunguu thomu na endelea kukaanga na mimina nyanya zilizo sagwa kisha koroga mchanganyiko wako.

Weka chumvi na royco kisha funika acha ichemke kwa dakika 1, mimina maharage yaache kwa dakika 1, mimina tui jepesi acha lichemke kwa dakika 3, mimina tui zito kisha yakoroge maharage yako kidogo acha lichemke kwa dakika 2.

Epua acha kiasi cha dakika 5 ndio uyapakue, unaweza kula na wali, ugali au mikate

## MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

# Andaa nyumba ya kijijini kwenu

MSIMU wa sikukuu hasa kipindi hiki cha mwisho wa mwaka, unawafanya watu wengi hasa wa mjini kwenda kutembelea ndugu na jamaa vijijini.

Hii ni kwa wale waliozaliwa na kukulia kijijini; japokuwa kuna wanafamilia wachache ambao hutoka kijijini kwenda kusherehekea msimu wa mwisho wa mwaka kwa ndugu zao waishio mjini.

Ukurasa huu leo unazungumza zaidi na wale waliopanga kwenda kijijini kwa mapumziko ya msimu huu wa mwisho wa mwaka.

Kwanza, hakikisha unapanda miti ya asili inayostawi katika kijiji chenu. Hii ni mizuri kwa utunzaji wa mazingira na mingine ni tiba ya ardhi kwani mingi inaweza kuvuta maji, huku majani yake yakiwa mbolea nzuri kwenye shamba. Usisahau pia kupanda ile ya matunda.

Inashauriwa kuwa miti ya matunda ipandwe pia kwa kuzingatia hali ya hewa ya eneo husika, usije ukapanda parachichi kwenye eneo linalostawi stafeli. Kadhalia, wageni wajiandae kwa kupanda mboga ambazo watazitumia wakati wa likizo.

"Watu wazingatie sana upandaji wa miti ya asili ya maeneo yao, kuliko miti migeni ambayo baadhi inaweza kuwa ni magugu badala ya kuleta faida inayotarajiwa. Suala la mboga, ukishajua siku utakayoenda kijijini, unawaandaa watu wa nyumbani kwako kwa kuwatumia mbegu ili wakuandalie mboga nzuri za majani," anashauri mwanasayansi ya mazingira, Brigitha Didas.

Anaongeza: "Kwa wazazi wanaopeleka watoto kijijini, hakikisha kila mmoja anapanda mti wa kivuli wa asili au wa matunda. Hii itamwachia kumbukumbu nzuri hasa ya utunzaji wa mazingira, lakini pia itamwongezea furaha wakati mwingine atakapofika kijijini na kuona mti wake ukikua au akachuma tunda."

Anasema msimu wa sikukuu unaweza kutumiwa pia na wanakijiji kuandaa vyakula hasa mbogamboga ili wageni wazinunue.



Na Elizabeth Zaya



# Mbinu za kupambana na mchwa kwenye nyumba

MCHWA ni miongoni mwa wadudu hatari kwenye uharibifu wa nyumba.

Mdudu huyo amekuwa tishio kubwa katika ustawi wa nyumba na husababisha uharibifu mkubwa asipodhibitiwa.

Ziko mbinu mbalimbali za kupambana na mchwa huyo baada ya kujenga nyumba ambazo zinatajwa na mtaalam Leonard Pandamali.

Anasema namna ya kudhibiti mchwa kwenye nyumba baada ya ujenzi na kabla ya kuanza kuitumia ni lazima yote inyunyiziwe dawa ili kuua mazalia yote ya mdudu huyo.

Pondamali anasema kudhibiti mdudu huyo wakati tayari unaitumia nyumba kunaweza kuleta usumbufu kidogo tofauti na ilivyo kwa nyumba ambayo haijaanza kutumika.

Anashauri kwamba ni vyema mtumiaji au mmiliki wa nyumba kuweka utaratibu na mazoea ya kuweka dawa kila baada ya muda fulani kupita.

"Kabla ya kutumia dawa hizi za kuilinda nyumba yako dhidi ya mchwa ni vema ukapata ushauri wa mtaalamu wa ujenzi au kilimo na mifugo. Kuna aina nyingi za dawa zinazotumika kwa sasa na bado nyingine zinaendelea kubuniwa kuendana na ukuaji wa sayansi na teknolojia ya utengenezaji wa dawa.

"Ni vyema kutumia dawa kwa kuzingatia maelekezo ya mtaalamu au mzalishaji wa dawa hizo kwa sababu hazifanani katika mbinu za matumizi, hivyo usiige tu kutoka kwa wengine, ni vema kupata kwanza ushauri," anasema.

Anaelekeza kwamba kabla ya kuweka dawa kwenye nyumba, mtu anapaswa kusafisha mifereji na










kuhakikisha kwamba hakuna bomba zinazovuja ikiwamo kukausha maeneo yote yenye unyevunyevu.

Pia anasema kuweka dawa kwenye maeneo yote ambayo ni njia au makazi ya mchwa, na ambayo ni chanzo hata kama hakuna mchwa wanaoonekana.

Jambo lingine. anasema ni kung'oa na kuondoa mbao zote zilizoharibiwa na mchwa na kuweka nyingine pamoja na kutoruhusu mbao zozote zigusane na udongo wowote au unyevunyevu kwa muda mrefu na kuziba matundu yote kwenye sakafu na kuta.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
HALO YA FEI
USINICHULIE NDIO KWANZA NNA MIAKA CHINI YA THALAASINI
SHIKAMOO MZEE
DALA - DALA
OLE WAKO WAIFU WANGU ANGEKUWEPO
JUKWAANI
WE BABA KEI TUNATAKA HELA YA SUKARI NA VITAFUNIO ALAFU MANGI ANATUDAI TULIKOPA UNGA
ONGEZA SAUTI ZAIDI MAJIRANI HAWAJASIKIA
ENZI HIZO NILIVOKUWA 'BAUNSA' NILIWAHI KUBEBA ROLI ISUZU NA MCHANGA WAKE
ILI STORI INOGE NTAZAME USONI KAKA MKUBWA
DAH! HII LEO SIJUI KILANGA GANI KIMENTUMA
NATAKA NIJUE NYIE WATUMISHI WA DALADALA ZA NCHI GANI? MAANA HII STAILI HAPA KWETU IMEBAKI HISTORIA
LAKINI AFANDE TAMBUA KUWA HISTORIA HUWA INAJIRUDIA
NIJISEMEE UKWELI TU, SISI WATARAZAKI RIZKI TUNAJITUNDIKA HIZI OVASAIZI TUNAGONGA DEBE TUNADAKISHWA 'MIA MBILI BASI'
SHOSTI TUMEMKOMESHA MWENYEKITI WA VIKOBA HARUDII TENA!
CHEZEA SISI... KATUZULUMU HELA ZETU MILIONI SITA, NA SISI TUME-MCHUNA MUMEWE ALFU'SALASINI
'NGUO ZA WATEJA'
DOBI
TUONE SASA MIMI NA MVUA NANI ZAIDI... NTAKAPOLIKUTA JUA POPOTE NAZIANIKA

# Scholz, Putin wazungumza Ukraine yakasirishwa

**KYIV,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amesema amesikitishwa na mazungumzo yaliyofanywa kati ya Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz na Rais wa Russia, Vladimir Putin.

Akizungumza kupitia video, Zelensky amesema mazungumzo ya viongozi hao yalifanyika kwa njia ya simu hayawezi kufikia popote.

Alisema hatua hiyo itafanya mambo kuwa magumu na kwamba mazungumzo kati ya Kansela Scholz na Rais Putin huenda yakafungua njia ya mazungumzo zaidi, jambo ambalo Putin amekuwa akilitafuta kwa muda mrefu.

Zelensky hata hivyo alikiri kwamba alifahamishwa mapema kuhusu mazungumzo ya viongozi hao.

Kansela Scholz alizungumza na Putin kwa muda wa saa moja juzi, ikiwa ni mazungumzo ya kwanza kati ya viongozi hao wawili katika kipindi cha miaka miwili.

Kulingana na Msemaji wa serikali ya Ujerumani, Steffen Hebestreit, Kansela Scholz aliitaka Russia kuondoa wanajeshi wake kutoka Ukraine, kumaliza vita na pia kumtaka kufanya mazungumzo na Zelensky kwa lengo la kupata amani ya kudumu.

Kansela Scholz pia alisisitiza uungaji mkono wa nchi yake kwa Ukraine katika mapambano dhidi ya uvamizi wa Russia ambao unaelekea kuwa wa muda mrefu na kwamba Russia ifikirie muda upo upande wake.

Wakati wa mazungumzo yake alimuonya Putin kwamba kupelekwa kwa wanajeshi wa Korea Kaskazini kwa ajili ya mapigano nchini Ukraine au Russia ni kuuzidisha mzozo huo. Muda mfupi kabla ya mazungumzo hayo, kiongozi huyo wa Ujerumani alisisitiza bungeni kwamba nchi yake haitoipatia Ukraine makombora ya masafa marefu ya Taurus, ambayo imeomba mara kwa mara.

Kulingana na Ikulu ya Russia, Rais Putin alielezea nia yake kwa Scholz kufanya mazungumzo lakini chini ya mazingira yenye maslahi kwa Russia.

Alidai kwamba utatuzi wowote wa mzozo huo lazima uzingatie masilahi ya usalama ya Russia na pia kuzingatia ukweli wa maeneo iliyoyatwaa ya mashariki na kusini mwa Ukraine.

Baadhi ya masharti ya Rais Putin ni Ukraine kuacha wazo la kujiunga na Nato

**DW**



Polisi na walinzi wa kibinafsi wakijaribu kuwaondoa wachimbaji haramu kwenye shimo la mgodi wa dhahabu katika eneo la Stilfontein, Afrika Kusini, juzi. **PICHA: AP .**

## Wachimbaji madini Afrika Kusini waendelea kukwama mgodini

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

POLISI nchini Afrika Kusini wanaendelea kulinda eneo la migodi ya madini ambako mamia ya wachimbaji wamekwama chini ya ardhi wakihofia kukamatwa katika operesheni ya kupambana na uchimbaji haramu.

Taarifa iliyotolewa na polisi ilisema zaidi ya wachimba migodi 400, maarufu kama "zama zama", wamejificha kwenye kina cha mgodi huo wa dhahabu ambao hautumiki.

Ni jambo la kawaida nchini HYPERLINK "https://www.rfi.fr/sw/lebo/afrika-kusini/" \t "_self" Afrika Kusini, migodi ambayo haitumiwi tena na makampuni ya uchimbaji madini, inachimbwa kinyume cha sheria na wachimbaji wadogo.

Migodi hiyo ina kina kirefu inayofikia hadi mita 2,000, na mashimo mengi zaidi ya kilomita kadhaa. Wakati mwingine wachimbaji hutumia miezi kadhaa kuchimba ndani ya migodi hiyo bila kutoka nje.

Njia ya kutoka ya mgodi huo imezungukwa na kamba ya usalama, huku magari kadhaa ya polisi yameegeshwa pande zote.

"Tunakuja kila siku kuanzia saa 12 asubuhi. Kawaida tunawapa chakula, lakini sasa hatuwezi. Tunaishi kwa neema ya mgodi huu, tunapata chakula kwa ajili ya mgodi baada ya wanaume hawa kuingia kufanya kazi. Kwa mfano, mume wangu hunilipia ada ya masomo ili nisome. Sasa amenaswa huko, siwezi tena kulipia masomo yangu," anaeleza mwanamke mmoja.

**DW**

# Hamas yakubali kumaliza vita Ukanda wa Gaza

**NEWYORK,** MAREKANI

WAKATI Umoja wa Mataifa umesema hali bado si nzuri katika ufikishaji wa misaada kwenye maeneo ya Ukanda wa Gaza.

Kundi la Hamas limesema liko tayari kusitisha vita.

Zoezi la kufikisha misaada katika Ukanda wa Gaza, linaendelea kuwa gumu huku usafirishaji wa misaada hiyo hadi katika eneo la kaskazini lililozingirwa na vikosi vya Israel kwa sasa hauwezekani.

Hata hivyo, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken na Waziri wa Ulinzi Lloyd Austin katika barua yao ya Oktoba 13 kwa Israel walimpa mshirika wao huyo orodha ya hatua mahususi ambazo ilihitaji kuzifanya ndani ya siku 30 ili kukabiliana na hali inayozidi kuwa mbaya katika eneo hilo.

Hata hivyo, Israel yenyewe kwa upande wake imesema inajitahidi kusaidia kufikishwa misaada ya kibinadamu na mahitaji mengine huko Gaza.

Hata hivyo msemaji wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu, Jens Laerke alipoulizwa swali kwenye mkutano na waandishi wa Habari mjini Geneva alijibu kuwa hakuna maendeleo katika usambazaji wa misaada na hali imezidi kuwa mbaya.

"Kwa mtazamo wetu zoezi la upatikanaji wa misaada liko katika kiwango cha chini sana, machafuko, mateso, kukata tamaa, vifo, uharibifu na watu wanapoteza makazi yao kwa kiwango cha juu ni mambo yanayotia wasiwasi mkubwa na hasa hali ilivyo katika eneo la kaskazini mwa Gaza, ambalo sasa limezingirwa. hali huko inakaribia kuwa haitawezekana kufikisha msaada huko." Alisema.

Aidha, Ofisa mkuu wa Hamas ambaye ni mjumbe wa ofisi ya kisiasa ya kundi hilo, Bassem Naim, alisema kundi hilo liko tayari kwa usitishaji vita katika na amemtaka Rais mteule wa Marekani, Donald Trump, kuishinikiza Israel kukomesha vita.

Naim aliliambia shirika la Habari la AFP kwamba Hamas iko tayari kufikia makubaliano ya kusitisha vita ikiwa pendekezo la kusitisha mapigano litawasilishwa na kwa sharti kwamba litaheshimiwa na Israel.

Alisema Hamas imewafahamisha wapatanishi kwamba inaunga mkono pendekezo lolote litakalowasilishwa kwao ambalo litawezesha vita kusimama na Israel kuwaondoa wanajeshi wake kutoka Ukanda wa Gaza, kuwaruhusu watu waliokimbia vita kurudi kwenye makazi yao, kuachiwa mateka wa Israel na pia wafungwa wa Kipalestina.

**DW**

HABARI/SAFU

# Mwinyi awafunda vijana kuheshimu wazazi

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (pichani) amewataka vijana kuwathamini wazazi wao na kuwatendea mema ili kupata baraka za Mwenyezi Mungu.

Amesema ni wajibu na ni jambo jema kwa vijana ambao wazazi wao wako hai kuishi nao kwa huruma na upendo na kuwaombea dua wale waliotangulia mbele ya haki kwa kuwa kuna fadhila nyingi kwa kutekeleza jambo hilo.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano Ikulu, Zanzibar, ilisema Dk. Mwinyi alitoa rai hiyo juzi alipojumuika na waumini wa dini ya Kiislamu katika ibada ya swala ya Ijumaa iliyofanyika kwenye Msikiti wa Maungani, Wilaya ya Magharibi B.

Akitoa hotuba ya Ijumaa, Khatibu wa Msikiti wa Ijumaa wa Maungani, Sheikh Suleiman Mwinchumu Suleiman, aliwasisitiza waumini hao kuwa karibu na wazazi wao pamoja na kuzungumza nao kwa maneno mazuri na kuacha hasira juu yao kama ilivyoamrishwa na miongozo ya dini ya kiislamu.

Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Mufti, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema ni vyema kwa waumini wa kiislamu kufahamu dua ya kuwaombea wazee na kuitekeleza kila wanapopata fursa ya kufanya hivyo ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Wakati huohuo, Dk. Mwinyi baada ya sala ya Ijumaa, aliendeleza utaratibu wake wa kuwatembelea wananchi na kuwajulia hali Wagonjwa katika maeneo mbalimbali.

Aliowatembelea juzi ni aliyekuwa Mbunge na Naibu Waziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mshauri wa Rais wa Zanzibar Awamu ya Saba, Dk. Maua Abeid Daftari, anaeishi Beit Ras, wilaya ya Magharibi A.

Wengine ni mkongwe wa sanaa za Filamu na Maigizo Zanzibar, Mwanamwema Khamis Juma, maarufu kama Bi Njiwa, Halima Muhamed, mjane wa aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini Kichama, Marehemu Borafya Silima wanaoishi Mwera Mtofaani.



# Waziri azindua miradi ya mil. 904/- Serengeti

**Na Happiness Shayo,** SERENGETI

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana, amezindua miradi ya kuendeleza utalii ikiwamo ya Barabara ya Utalii yenye urefu wa kilometa 22 uliogharimu takribani Sh. milioni 761.3.

Mradi mwngine ni ujenzi wa vituo viwili vya kupokea na kukagua wageni (Ikona Gate na Visitors Gate) uliogharimu Sh. milioni 143.5 katika Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Ikona, wilayani hapa.

Uzinduzi huo ulifanyika juzi katika Jumuiya ya Hifadhi ya Ikona wilayani Serengeti.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi huo, Balozi Chana aliitaka jumuiya hiyo kuisimamia na kuitumia vyema miradi hiyo kwa malengo yaliyokusudiwa ya kukuza utalii huku akisisitiza maadili katika utendaji kazi.

"Natoa rai kwa wafanyakazi kuwa waadilifu katika kutekeleza majukumu ya ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za taifa," alisisitiza Balozi Chana.

Aidha, Waziri alipomngeza menejimenti na jumuiya ya Ikona huku akitoa rai kuendelea kushirikiana kwa karibu na halmashauri za wilaya, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kutekeleza majukumu yake.

Naye Mhasibu wa Jumuiya ya Ikona, Mariam Magessa, alisema jumuiya hiyop, tangu kuanzishwa kwake, imepunguza matukio ya ujangili, hivyo kusababisha ongezeko la wanyamapori huku ikivutia shughuli za utalii na wawekezaji.

"Matokeo chanya ya uhifadhi yamesababisha kupata wawekezaji tisda, wanane kati ya hao wamewekeza kwenye utalii wa picha na mmoja kwenye utalii wa uwindaji," al;lisema Magessa na kusema hiyo imekuwa sehemu ya mapato ya jumuiya hiyo.

Jumuiya ya Ikona ilianzishwa mwaka 2005 kwa lengo la kuendeleza uhifadhi na usimamizi endelevu wa maliasili na vivutio vya utalii kama njia ya kukuza uchumi na hivyo kupunguza kiwango cha umaskini kwa wananchi wanaoishi katika vijiji wanachama.

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Ugomvi wa mke na mume kwa nini waingilia?



**Na Adam Fungamwango**

**Ndiyo maana mwanamuziki Mbaraka Mwinshehe aliwahi kutunga wimbo akauita 'Ugomvi Mke na Mume'.**

MARA nyingi mambo ya ugomvi wa mke na mume yana mambo mengi. Ndiyo maana wazee wa zamani wanasema ugomvi wa mtu na mpenzi wake, au mumewe usiuingilie.

Wanajua kuna sababu tu ndogo inayosababisha hilo, ambayo kwa wakati huo haijarekebishika, lakini dosari zikiondolewa, wataendelea kupatana na walioingilia watabaki na aibu.

Wanaposema usiingilie, si kama wakipigana watu wasiamue, au wanapopeleka kesi kwa wakubwa wasiiamue, la hasha. Maana yao ni kwamba upande mmoja kati ya hao wawili. Yaani unamsaidia mume kumshukutumu mke, au unakuwa upande wa mke kumuona mume amekosea.

Hili ni kosa kubwa sana. Kinachotakiwa ni kuwaamulia na kuwataka waache mzozo, kutupiana maneno, kupigana, au mmoja kumpiga mwingine.

Nitoe mfano mmoja tu, kuna mwanamke alikuwa anaumwa huko Kisemvule pembezoni mwa Dar es Salaam.

Mume wake akawa hamjali hata kumpeleka hospitali akashindwa. Mke kwa hasira akawapigia simu ndugu zake, ambao walikwenda huko kwa hasira na kumtukana sana mwanamume.

Wakamchukua ndugu yao na kumpeleka Kunduchi kwa mmoja wa ndugu, akatibiwa.

Kabla hata hajapona vizuri, mke akatoroka na dawa zake kurudi kwa mumewe. Kumbe siku zote walikuwa wakiongea kwa simu na kuyajenga. Ndugu waliomtibia na kumtukana jamaa wakabaki midomo wazi.

Ndiyo maana mwanamuziki Mbaraka Mwinshehe aliwahi kutunga wimbo akauita 'Ugomvi Mke na Mume'.

Akaonya kabisa kuingilia ugomvi wao kwani baadaye watu wanaweza kupata lawama. Haya ndiyo mashairi wa wimbo huo yenye mafunzo makubwa kwenye jamii.

*"Wanapogomba ooo, mtu na mke wake ndani ya nyumba, usiingilie kati kabisa ugomvi wao. Utakuja pata balaa we kijana, ya kusingiziwa mengi na isitoshe, leo unagombombelezea mwisho wake utapata lawama.*

*"Hayo yashike kichwani, usijitie kimbelembele, usipoelewa neno lolote usijitie wajua. Wengine hawana masihara, hata hasira hazijamuisha wewe wamtibua, hatari wajitakia ooo.*

*Kinachokuuma kitu gani, ugomvi yeye na mke wake, waingilia kwa nini, waitafuta lawama. Hatari wajitakia, waitafuta lawama. Ugomvi yeye na mke wake, waingilia kwa nini? Ukipigwa panga mbele ya hakimu utasemaje?"*

Haya ni mashairi ya wimbo huo uliotungwa na kupigwa na mwanamuziki huyo miaka ya 1970, ambapo maudhui yake hadi leo yanaishi.

Hii ndiyo tofauti ya tungo za zamani na za sasa. Tungo za sasa pamoja na kwamba nyingi ni za mapenzi, lakini ni za kufikirika zaidi.

Unapotungwa wimbo uliomhusu mtu fulani, au kitu fulani cha kijamii hata kama kilitokea miaka ya 1910, lakini kwa sasa uliuhusu jamii, basi maudhui yake yataedelea kuishi kwa sababu maisha yanaendelea kuwa ni yale yake.

Watu wanazaliwa, wanakua, wanaoa, wanaolewa, wanazaa na hatimaye wanakufa. Kwenye maisha kuna vitu vingi ambavyo vinafanana kwa asili ya binadamu.

Kilichompata mtu wa miaka hiyo, ni lazima kimpate wa miaka hii. Hakuna kipya zaidi duniani, yote yanajirudia tu. Matatizo ya ndoa, kuachwa, kutorokwa, kuachana, roho za kwa nini, mgogoro wa wake na mawifi, yote yalianza karne na karne na hadi leo yanaendelea na yataendelea kuwepo.

Ndiyo maana wanamuziki wanaotunga nyimbo kwenye maeneo haya, zinaendelea kuishi na kufundisha, licha ya kwamba wengi wao wameshafariki.

*Tuma meseji 0716 350534*

# HADITHI

## Nyuma ya Pazia-9

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

KESHO yake asubuhi aliamkia kwa bosi wake, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum kwa ajili ya suala hilo. Akamuelezea kila kitu bila kuacha chochote hata chembe. Alichoomba afande Chacha ni kubadilishiwa askari wenzake. Kwa jinsi alivyoona kamanda ni kwamba akifanya hivyo ataonekana kama imani na wale wawili badala yake anayo kwa mmoja tu ambaye ni Chacha. Aliona haitokuwa vyema kwani hana uhakika kati ya wote ni nani anavujisha siri. Alichofanya alimwambia amletee faili hilo na yeye ndiyo sasa atajua nini afanye.

Baada ya Chacha kutelekeza amri hiyo, alimtaka aendelee na shughuli zingine kwani faili hilo atamkabidhi mtu mwingine.


Aliwaza na kuwazua ampe mtu wingine kwenye ofisi yake, lakini aliona ni kama atakuwa amewafanya wengine pale hawajui kazi, lakini pia hata yeye hakujua ni nani anavujisha siri, inawezekana siyo hao ila ni mmoja wa watu waliomo kwenye ofisi yake. Kupeleka kwa mtu wa kanda nyingine ya Dar es Salaam aliona haiwezekani. Mwishoni wazo likamjia la kumpigia simu bosi mwenzake wa Idara ya Usalama ambaye hufanya naye kazi kwa karibu.

Alimkumbushia sakata la mtoto kutekwa na kwamba kumetokea utata kwenye ofisi yake, hivyo anachotaka asaidiwe kupewa mtu mmoja ambaye anatafanya kazi ya kupeleleza vitu viwili.

Kwanza alipo mtoto aliyetekwa na kukamatwa na wahusika wote. Pili kutegua kitendawili cha nani alikuwa anavujisha siri katika majaribio mawili ya kwanza ya kukamatwa kwao.

"Afande, nitakupa kijana mmoja hivi, kwa hilo uliloniambia ni jambo dogo sana kwake." Alisema bosi hiyo na kumshtua wenzake "Unasema kweli?" "Si hilo tu uliloniambia? Au kuna lingine? "Hilo tu mheshimiwa." "Basi ondoa shaka, Huyu kijana hata kama kuna lingine angetatua tu. Ameisaidia nchi kwa mambo mengi makubwa, sembuse hili tu la kijamii?" Haya mheshimiwa namhitaji hata kesho aje ili nimpe mrejesho, faili na nimkabidhi kwa wahusika ili aanze kazi." Okay, nikamwita asubuhi na kumwambia hilo."

Ahsante sana mheshimiwa. Karibu Kamanda. Tayari alikuwa ameutua mzigo ambao ulikuwa unataka kumwelemea. Kelele za wananchi kuhusu kutekwa kwa mtoto kulimsumbua na alidhani kina Chacha alikuwa wamefika mbali, kumbe walikuwa wanapigwa chenga na watekaji. Alimwamini mwenzake Bosi wa Usalama kwani hajawahi kumwangusha hata mara moja.




**"Na kila wanapokwepa, wanamwambia baba mzazi wa mtoto nini kimetokea mpaka wao wameshindwa kwenda kuuchukua mzigo, wanamwambia arudi nao. Jeshi la Polisi limekuwa kilitoa msaada ya pesa hizo Sh. Milioni 15 zinazotakiwa na watekaji, lakini kila zinapopelekwa jamaa wanajua kuwa polisi wanazifuatilia kwa ajili ya kuwakamata, hivyo hawaendi."**

Bosi wa Usalama naye baada ya kumsikiliza kwa makini alijua nani ya kumpa ili kuutatua mkasa huo tata.

Alitabasamu mwenyewe akimfikiria mtu ambaye atamkabidhi kazi hiyo, kwani hupenda mno kupeleleza, kusaka na kukamata wahalifu kwenye mazingira magumu kama hayo.

"Kama alifanya kazi ngumu za kuisaidia nchi, ndani na nje ya Tanzania, hii ni rahisi zaidi kwake. Nadhani haitochukua hata wiki mbili." Akajisemea mwenyewe.

Akainua mkono wake kutaka kumpigia simu, lakini kama kuna sauti ikamwambia asubiri mpaka kesho yake kwani muda ulikuwa umekwenda mno. Akaangalia saa yake ya mkononi. Ikamuonyesha ni saa 10:00 jioni, muda ambao hata yeye mwenyewe anatakiwa aondoke ofisini.

*************************************

"Faili lenyewe hili hapa, limeletwa muda si mrefu. Kifupi tu ni kwamba kuna mwanafunzi mmoja mdogo sana mwenye miaka sita, jina lake utaliona humo. Ametekwa na watu wasiojulikana. Mpaka sasa hajapatikana. Lakini watekaji wamekuwa wakimpigia simu baba mzazi wa mtoto kutaka fedha. Lengo la utekaji huu ni jamaa hao kutaka pesa. Kwa bahati mbaya sana wanaonekana wana mtandao mpana ambao unasababisha kuwakamata kwake kuwa kugumu.

Hawa jamaa huwa wanampigia baba mzazi tu kutaka pesa. Na kila wakipiga wanatumia namba tofauti na wakiitumia hawaitumii tena. Ukienda kusachi namba unaambiwa haijasajiliwa. Ajabu ni kwamba wakipanga sehemu ambayo wanataka zipelekwe wanajua kama wanafuatiwa na askari.

Mara mbili wamekwepa mtego wa kunaswa na polisi," alisema Bosi na kumwangalia kwa bashasha aliyekuwa anampa habari hiyo.

"Na kila wanapokwepa, wanamwambia baba mzazi wa mtoto nini kimetokea mpaka wao wameshindwa kwenda kuuchukua mzigo, wanamwambia arudi nao. Jeshi la Polisi limekuwa kilitoa msaada ya pesa hizo Sh. Milioni 15 zinazotakiwa na watekaji, lakini kila zinapopelekwa jamaa wanajua kuwa polisi wanazifuatilia kwa ajili ya kuwakamata, hivyo hawaendi."

"Okay, nimekuelewa Bosi. Ni hivyo tu, au kuna kingine? Nadhani ni hivyo tu. Vingine wewe ndiyo utatuambia mwisho wa kazi hii."

Aliondoka maeneo ya Posta kwenye kwenye ofisi za bosi wake na kuelekea Mikocheni zilipo ofisi zake.

Alipofika jambo la kwanza alianza kupitia faili la mkasa huo alilopewa.

Ndipo alipogundua kuwa baada ya mtoto Macaire kutekwa, lengo la watekaji lilikuwa ni pesa.

Matukio mawili ya kupeleka pesa kwa watekaji hayakufanikiwa. Sababu kubwa ilikuwa ni watekaji kufahamu kuwa wanafuatiliwa na askari polisi ambao wameweka mtego. Pesa zinatolewa na polisi kwa sababu kuwakamatisha hazifanyi kazi kwa sababu watekaji wanakuwa wanajua kuwa pesa hizo ni za polisi na pia wanafuatiliwa, hivyo kutofika eneo la tukio ambalo walikuwa wanapanga wenyewe.

Hisia zikaanza kuwa labda ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Tom Academy, Kisanga, anaweza kuwa anahusika kwa njia moja ama nyingine. Wakaamua kumuweka kando na kutomwambia chochote.

Hata hivyo bado watekaji wakawa wanapata taarifa ya vyote vinavyofanyika. Alichogundua pia ni kwamba watekaji humtumia baba wa mtoto aliyetekwa tu, Macky kutaka pesa na si mtu mwingine yeyote. Alichofanya siku ya kwanza ni kwenda Mbezi Beach kwenye shule ambayo mtoto Macaire alitekwa.


Akiwa anaendesha gari yake ndogo aina ya Volvo, XC60 alifika shuleni hapo na kuonana na mwalimu Kisanga. Alijitambulisha kama ni askari polisi wa kawaida tu ambaye anapeleleza kesi hiyo.

Alimuuliza maswali kadhaa ambayo aliona yangeweza kumfanya aanze kwa kuanzia. Na hii ni baada ya kuambiwa kuwa alikuwa mtu wa kwanza kutoambiwa chochote kuhusu taarifa za kupeleka pesa kwa watekaji ili kuangalia kama zinaweza kusababisha kumnasa anayetoa taarifa kwao. Kwa uzoefu wake hakuona kama mwalimu huyo anahusika kwa chochote.

Kwa sababu alikuwa na namba za baba wa mtoto aliyetekwa alimpigia ili wakutane maeneo ya Ubungo jijini Dar es Salaam.

Eddy alimpeleka moja kwa moja ofisini kwake. Ambapo alikuwa anataka kumuuliza maswali mawili matatu ambayo anadhani yangeweza kumfanya kugundua kitu.

**Itaendelea Jumapili**



# TAMASHA LA WAHANGAZA WAISHIO DAR

**NA JUDITH JULIUS,** Ngara

WANANCHI wa kabila la Wahangaza wanaoishi Dar es Salaam hivi karibuni walifanya tamasha la kitamaduni lililoambatana na burudani mbalimbali za asili.

Wahangaza ambao wanatoka Wilaya ya Ngara mkoani Kagera, kwa kipindi cha miaka miaka 10 wanafanya tamasha hilo kwa lengo la kudumisha mila, taratibu na tamaduni za jamii hiyo.

Mwenyekiti wa umoja wa Wanangara wanaoishi Dar es Salaam, Idelphonce Mabamba, alisema licha ya kujumuika pamoja kuburudika kwa ngoma, vyakula na vinywaji vyenye asili ya kwao, wanajadiliana masuala mbalimbali ikiwamo maendeleo yao kupitia vikoba.

Chifu wa Wahangaza, Pius Balamba, alieleza kuwa ni vizuri kwa wanachama wa umoja huo kukutana kwa lengo la kujifunza mila na desturi za wazee waliotangulia mbele za haki.

Balamba alisema kuwa ni vema kuwepo utaratibu utakaoshuhudia wanachama hao wakikutana ili kuenzi mambo mazuri katika kabila lao na yaendelee kuenziwa na vizazi vijavyo.

# ‘Emorado’ ya Phantom Musica imekamilika

BENDI ya muziki wa Dansi la Phantom Musica International limekamilisha kurekodi wimbo mpya uliopewa jina la ‘Emorado’.

Mkurugenzi wa Phantom Musica International, Abdulfareed Hussein amesema wimbo ‘Emorado’ umeimbwa kwa lugha ya Kiswahili na Kireno na umetungwa na mwimbaji mkongwe Karama Regesu.

Ameongeza kuwa, dhamira ya kutumia lugha mbili ni ubunifu wa kimuziki ili kuongeza mvuto kwa wadau wa burudani wa muziki wa dansi.

“Emorado ni aina nyingine ya kazi za ubunifu kutoka Phantom Musica. Kutoka katika utaratibu wa kuwatumia wanamuziki wenye majina makubwa kutoka bendi mbalimbali nchini na sasa tumeingia katika mseto wa lugha” amesema Hussein na kuongeza.

“Mtunzi Karama Regesu ni kati ya wanamuziki wakongwe nchini mwenye utajiri wa kipaji mwenye uwezo wa kuzungumza kwa ufasaha lugha nyingi duniani na sasa ameamua kutumia Kiswahili na Kireno katika kibao hiki Emorado”.

Amesema kazi hiyo imerekodiwa katika Studio ya Amoroso Saundo iliyopo jijini Dar es Salaam na ndiyo wimbo wa kwanza wa albamu ya pili ya kundi hilo.



## ZISIKUPITE

### GUARDIOLA, MAN CITY SAFI

PEP Guardiola mwenye umri wa miaka 53, amefikia makubaliano ya kimsingi ya kuongezwa muda wa mwaka mmoja katika mkataba wake wa sasa na Manchester City. ***(Football Insider)***

### GORETZKA AGEUKA LULU

MANCHESTER United itakabiliana na ushindani kutoka kwa Union Berlin kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Leon Goretzka, mwenye umri wa miaka 29, ambaye anatatizika na hali yake katika Klabu ya Bayern Munich. ***(Team Talk)***

### NISTELROOY AITAKA COVENTRY

RUUD van Nistelrooy ametuma ombi la kuwa Kocha Mkuu wa Coventry City baada ya kuacha nafasi yake kama kocha msaidizi wa Manchester United. ***(Talksport)***

### JESUS AGOMBEWA EPL

KLABU ya Fulham imeungana na wapinzani wao wa London, Brentford kumwinda mshambuliaji wa Botafogo na Brazil, Igor Jesus, 23. Newcastle United na Nottingham Forest pia zinavutiwa na mchezaji huyo. ***(TBR)***

### ANDERSEN ATAKIWA JUVE

JUVENTUS inamtaka beki wa Fulham na Denmark, Joachim Andersen, 28, na mlinzi wa Chelsea na Ufaransa, Benoit Badiashile (23).***(La Gazzetta dello Sport)***

### LAMPTEY ANUKIA WEST

WEST Ham inamfuatilia kwa karibu beki wa Brighton, Tariq Lamptey, 24, na ipo katika nafasi nzuri ya kuishinda Everton katika mbio za kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ghana kwa uhamisho wa bure. ***(Football Insider)***

### SPURS YAMTAKA LAMPTEY

KLABU ya Tottenham Hotspur pia inamtaka Tariq Lamptey kwa nia ya kuimarisha safu ya ulinzi ya Kocha, Ange Postecoglou, wakati wa uhamisho wa wacheziji wa Januari. ***(Teamtalk)***

### KVARATSKHELIA KUTUA BARCA

BARCELONA inavutiwa na winga wa Napoli na Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, 23. Mchezaji huyo anakadiriwa kuwa na thamani ya euro milioni 67. ***(Repubblica)***

### HUMMELS : NITASTAAFU

MLINZI wa Ujerumani, Mats Hummels, 35, huenda akaamua kustaafu ikiwa hatapata nafasi ya kuondoka AS Roma katika dirisha la usajili la Januari. ***(Sky)***

### SVERRE AKARIBIA UNITED

KLABU ya Manchester United inaamini huenda ikahitaji kufanya uamuzi wa kumnunua mchezaji wa Rosenborg, Sverre Nypan, 17, haraka iwezekanavyo ili wapate saini ya kiungo huyo wa kati wa Norway. ***(Givemesport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MABAO YA RONALDO YAING'ARISHA URENO

### Yatinga robo fainali UEFA, nahodha huyo afikisha mabao 135...

**LISBON,** Ureno

TIMU ya Taifa ya Ureno imetinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mataifa ya UEFA baada ya Cristiano Ronaldo kufunga mabao mawili katika ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Poland 5-1 katika mechi ya Kundi A iliyochezwa juzi usiku.

**Mabao hayo mawili ya Ronaldo yalimfanya kufikisha magoli 135 aliyoifungia Ureno.**

Rafael Leão alifunga bao la kwanza kwa kichwa kabla ya Ronaldo kufunga goli la pili dakika ya 72.

Wakiwa wenyeji wa mechi hiyo walifunga mabao matatu ndani ya dakika nane kupitia kwa Bruno Fernandes, Pedro Neto na Ronaldo kabla ya Dominik Marczuk kufunga goli la kufutia machozi kwa Poland dakika ya 88.

"Kipindi cha kwanza kilikuwa kibaya sana kwa kile tulichotaka kufanya, tulipoteza umakini na kuchanganyikiwa. Lakini kipindi cha pili kilikuwa kizuri zaidi ambacho nimeona," alisema Kocha wa Ureno, Roberto Martinez.

"Tumebadilisha mawazo na kuongeza nguvu na kusaidiana. Hatukuruhusu Poland kucheza."

Ureno ambayo haijapoteza inaongoza kundi hilo ikiwa na pointi 13, sita mbele ya Croatia, ambayo ilipoteza kwa kufungwa bao 1-0 na Scotland ambayo bado iko mkiani lakini sasa inalingana pointi nne na Poland iliyo nafasi ya tatu.

Poland itawakaribisha Scotland hapo kesho wakati Ureno itasafiri kwenda Croatia.

Poland hawakuwa na mfungaji wao bora wa muda wote, Robert Lewandowski, ambaye ana jeraha la mgongo, lakini walikuwa wepesi kutengeneza hatari na walijaribu mara tatu kulenga goli kabla ya mapumziko ikilinganishwa na wenyeji.

## HABARI MICHEZO




# SALAH AFICHUA USHAURI WENGER

**LIVERPOOL,** England

MOHAMED Salah ameeleza kwa kina mazungumzo aliyofanya na aliyekuwa Kocha wa Arsenal, Arsene Wenger, ambapo Mfaransa huyo alimpa ushauri mzuri fowadi huyo wa Liverpool.

Mchezaji huyo wa Misri amekuwa mmoja wa wachezaji wa kuogopwa zaidi katika Ligi Kuu England kwa miaka saba aliyokaa Anfield, akifunga zaidi ya mabao 200 kwenye michezo 366 aliyoichezea klabu hiyo.

Ustadi wake uwanjani umedhihirisha hadhi yake kama mmoja wa mawinga bora zaidi duniani, akiwa nyuma ya Bukayo Saka katika asisti za ligi hadi sasa msimu huu. Wakati Salah amecheza chini ya makocha maarufu kama vile Jurgen Klopp - ambaye aliondoka Merseyside mapema mwaka huu - ni maneno ya bosi Wenger ambayo yameweka nafasi katika akili yake.

"Nilipata ushauri kutoka kwa Arsene Wenger hapo awali," alisema akikiambia kituo cha televisheni cha Liverpool.

"Alikuwa Melwood (uwanja wa mazoezi wa Liverpool) wakati huo, kisha nikamuuliza kuna tofauti gani kati ya mchezaji mzuri na mchezaji mzuri sana.

"Alisema, "Nadhani mchezaji mzuri sana huwa anazingatia mchezo. Hata kama hana kasi, anabaki kwenye mchezo hadi dakika ya mwisho au hadi filimbi ya mwisho."

"Kwahiyo ni hivyo, nafikiri kwangu, najua kuna baadhi ya michezo sina kasi. Lakini huwa najikita kwenye mchezo ili kumaliza mambo."




# Ghana yashindwa kufuzu AFCON 2025

**LUANDA,** Angola

GHANA ilishindwa kufuzu Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), kwa mara ya kwanza tangu mwaka, 2004 baada ya kutoka sare ya 1-1 na Angola hapo juzi.

Black Stars ilihitaji ushindi katika mchezo wao wa mwisho wa makundi ili kuweka hai matumaini ya kufuzu kwa michuano hiyo itakayofanyika nchini Morocco mwakani.

Ghana, mabingwa mara nne wa Afrika, wamecheza katika matoleo 24 ya michuano hiyo.

Ni mabingwa mara saba pekee Misri (26) na mabingwa watetezi, Ivory Coast (25) ndio wameshiriki mara nyingi zaidi michuano hiyo.

Angola ambayo tayari imefuzu ilianza vyema mbele ya mashabiki wa nyumbani, lakini mkongwe wa Ghana, Jordan Ayew alianza kuwafungia wageni bao kwa mkwaju wa faulo dakika ya 18. M'Bala Nzola alipata nafasi ya kusawazisha kwa penalti, lakini shuti lake liliokolewa na golikipa wa Ghana, Abdul Manaf Nurudeen.

Angola iliendelea kusukumiza mashambulizi na Felicio Milson alisawazisha dakika ya 64. Ghana imesalia mkiani katika Kundi F ikiwa na pointi tatu pekee katika michezo mitano iliyocheza.

Walihitaji ushindi mara mbili kutoka mechi zao mbili za mwisho huku wakiwaombea wapinzani wao, Sudan yenye pointi saba wapoteze michezo yao yote miwili ya mwisho.

Wakati huo huo, winga wa zamani wa Hertha Berlin, Myziane Maolida, alifunga bao dakika za mwisho kwa Comoro na kuiwezesha kufuzu kwa ushindi wa magoli 2-1 dhidi ya Gambia. Ni mara ya pili kwa taifa hilo la kisiwa cha Bahari ya Hindi kufuzu kushiriki AFCON.

Zambia, Mali, na Zimbabwe zilifuzu mapema Ijumaa, huku Nigeria, Tunisia, Afrika Kusini, Uganda, Equatorial Guinea na Gabon zikinyakua nafasi zao siku ya Alhamisi.

# Pogba, Juventus rasmi wamalizana

**TURIN,** Italia

PAUL Pogba ataondoka Juventus baada ya klabu hiyo ya Ligi Kuu Italia maarufu Serie A, kuthibitisha kusitisha mkataba wake kwa maelewano.

Mkataba wa Pogba utamalizika rasmi Novemba 30, mwaka huu, Juventus walisema, na kisha atakuwa mchezaji huru.

"Klabu inamtakia kila la heri Paul kwa mustakabali wake wa kuendelea kucheza soka," ilisema taarifa ya klabu hiyo ya Turin.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alipunguziwa adhabu ya kufungiwa kucheza soka kwa miaka minne hadi miezi 18 na Mahakama ya Usuluhishi wa Michezo (CAS), mwezi uliopita.

Alifungiwa baada ya kugundulika alitumia dawa za kusisimua misuli zilizokatazwa michezoni, sasa inamaanisha ataweza kucheza tena soka kuanzia Machi mwakani, ingawa bado haijajulikana ni wapi atasajiliwa.

Mkataba wake na Juventus ulitarajiwa kumalizika Juni mwaka, 2026.

"Wakati wangu Juventus umefika mwisho," alisema Pogba katika taarifa yake mwenyewe.

"Imekuwa fursa nzuri kuvua jezi ya Bianconeri (Juve) na kushiriki wakati mwingi maalum pamoja.

"Ninathamini kumbukumbu tulizofanya. Wanaendelea kuishi. Hata katika nyakati ngumu zaidi katika mwaka uliopita, sapoti yenu ilikuwa muhimu na ninataka kuwashukuru mashabiki wa Juve ulimwenguni kote kwa huruma yao.

"Imekuwa ya kufurahisha kupata uzoefu kama huo, nyakati nyingi nzuri na wachezaji wenzangu kwa miaka mingi na ninawatakia mafanikio mema katika siku zijazo."

Pogba mwenye umri wa miaka 31, hajacheza tangu Septemba 3, mwaka jana.

Pogba alikuwa mchezaji wa soka ghali zaidi katika historia alipojiunga na Manchester United kutoka Juventus kwa ada ya euro milioni 105 hapo mwaka, 2016.



## Yanga hasira

INATOKA UK. 24

wanachama, mashabiki na wapenzi wa Yanga jezi zetu tayari zimefika na zitazinduliwa Novemba 20, mwaka huu, tunataka wakati watu wananunua tiketi basi, na jezi pia ziwe tayari sokoni zinauzwa.

Mechi itapigwa kuanzia saa 10:00 jioni, tunaamini ni muda ambao mchezo utaisha mapema ili watu warejee majumbani mapema kwa ajili ya kuamkia kazini Jumatano," alisema Kamwe.

Ofisa huyo alikanusha klabu yao kumwajiri aliyekuwa Kocha Mkuu wa KMC FC, Abdihamid Moallin, na kuongeza kocha wao msaidizi atatangazwa wakati wowote kuanzia sasa.

"Mmendika kuhusu Moallin, si kweli, hakuna ukweli, nawaambia leo (jana), naua hizo tetesi na taarifa, na Wanayanga wote ambao waliamini hiki kitu nawaambia rasmi si kweli, hakuna ambaye amewahi kumwona kocha wetu msaidizi, hakuna yoyote anayejua jina lake wala ubini wake, yupo hapa hapa nchini, hajui kiswahili la kingereza, anajua lugha ya kwao Poland tu," Ofisa habari huyo aliongeza.

Hata hivyo bado haijafahamika Moallin ambaye amebwanga manyanga ya kuifundisha KMC atajiunga na timu gani baada ya Gamondi kutimuliwa na msaidizi wake, Moussa Ndaw.

## Mpanzu aongeza nguvu Simba CAF

INATOKA UK. 24

kipa namba moja wa timu hiyo.

Lakred alionekana kuwa fiti, akifanya vitu ambavyo vimezoeleka na mashabiki wa timu hiyo akiwa langoni.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alisema ameomba mchezo huo wa kirafiki kwa ajili ya kuwaweka fiti wachezaji wake na kiushindani kwa sababu wanajiandaa na mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravo do Maquis kutoka Angola utakaochezwa Novemba 27, mwaka huu

kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Tumepata mchezo huu, pia mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Pamba Jiji pia utatupa taswira halisi ya ushindani. Tuna wachezaji ambao wapo katika vikosi vya timu za taifa, hivyo ni lazima wanaobaki nao wapate mechi za kujipima nguvu ili wote wakikutana wawe na levo moja ya fiziki," alisema Fadlu.

Taarifa zaidi zinasema Fadlu ameomba mchezo mwingine wa kirafiki kabla timu yake haijacheza mechi dhidi ya Pamba Jiji hapo Novemba 22, mwaka huu na alitamani kucheza dhidi ya Azam FC.

# SIMCHIMBA AIWEKA KILELENI GEITA LIGI YA CHAMPIONSHIP

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Geita Gold iliyoshuka daraja msimu uliopita, imezidi kujiweka katika mazingira mazuri ya kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Bigman FC katika mechi ya Ligi ya Championship iliyochezwa kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari ya Nyankumbu mkoani, Geita juzi.

**Ni ushindi wa sita kwa timu hiyo ambayo imefikisha pointi 20 na sasa inaongoza katika msimamo wa ligi huyo.**

Bao pekee katika mchezo huo lilifungwa na straika wao tegemeo na mchezaji bora wa Ligi ya Champioship wa Oktoba, mwaka huu, Andrew Simchimba, dakika ya 37, ambaye sasa amefikisha mabao sita kwenye orodha ya wafungaji wa ligi hiyo, sawa na Abdulaziz Shahame wa TMA.

Kinara wa mabao katika ligi hiyo ni Raizin Hafidh wa Mtibwa Sugar, mchezaji bora wa Septemba, mwaka huu akiwa naye amepachika mabao saba mpaka sasa.

Songea United, ikiwa kwenye Uwanja wake wa nyumbani wa Majimaji mkoani Ruvu yenyewe ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kiluvya FC hapo juzi.

Lilikuwa ni bao pekee la Andrew Chamungu, dakika ya 34 ya mchezo lililoipandisha timu hiyo hadi nafasi ya tatu ya msimamo ikifikisha pointi 18 baada ya kucheza michezo tisa, ikishinda mitano, sare tatu na kupoteza mmoja.

Mechi nyingine ilichezwa kwenye Uwanja wa Mnyanjani, Tanga katika Kituo cha Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), ambapo wenyeji, African Sports walikutana na kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Stand United.

Mabao yote ya washindi yalifungwa na Msenda Msenda, akiipandisha timu yake hadi nafasi ya nne ikiwa na pointi 18 kibindoni sawa na Songea United, lakini ikizidiwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

"Tunashukuru ushindi huu wa ugenini, umetufanya turudi tena katika mstari wa kusaka nafasi ya kupanda Ligi Kuu," alisema mfungaji huyo.

Msenda aliongeza wachezaji wa timu hiyo wamejipanga kupambana katika kila mechi ili kufikia malengo yao ya kupanda daraja.

Alisema ndoto zao ni kuona wanafanya vizuri katika kila mechi ili kukata tiketi ya kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu ujao.



Mkufunzi wa VAR wa FIFA na CAF, Janny Sikazwe (wa pili kushoto waliokaa), akiwa na Wakufunzi Watanzania baada ya kumaliza mafunzo ya siku tano ya kutumia vifaa vya usaidizi vya uamuzi vya video yaliyofanyika jijini, Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# *Washiriki Kilimanjaro Marathon waitwa*

**Na Mwandishi Wetu**

WAANDAAJI wa mbio za Kimataifa za Kilimanjaro wamewakumbusha washiriki zimebakia siku chache lakini wakiwataka kunufaika na punguzo za bei ya usajili lililotolewa kuelekea mbio hizo zitakazofanyika Februari 23, mwakani Mjini Moshi, imeelezwa.

Ili kupata punguzo, mshiriki atatakiwa kujiandikisha kabla ya Desemba 12, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na waandaji wa mbio hizo imesema dirisha linalotoa unafuu wa ada ya ushiriki bado liko wazi na washiriki wameaswa kujiandikisha mapema ili kuepuka adha ya mrundikano wa dakika za mwisho au kukosa fursa ya punguzo hizo.

"Kipindi cha washiriki kunufaika na punguzo maarufu kama 'ndege alewahi' kilianza Oktoba, 21 mwaka huu, ambapo kinatarajiwa kumalizika usiku wa manane Desemba 12, mwaka huu.

Hii inatumika kwa makundi yote ya mbio zikiwao Kilimanjaro Premium Lager (kilomita 42), kilomita 21 (Tigo Kili half marathon) na kilomita tano ambazo ni Fun Run," ilisema taarifa hiyo.

Iliongeza ili kuongeza usalama mbio hizo zitakazofanyika kuanzia kwenye Uwanja wa Chuo cha Ushirika Moshi, zitafuata kanuni rasmi za Shirikisho la Riadha la Kimataifa (IAAF).

"Lengo la kuzingatia kanuni hizo za IAAF ni kuhakikisha washiriki wanafurahia muda wao wakati wa kushiriki mbio hizo kwa kuepuka msongamano mkubwa na wakati huo huo kuhakikisha huduma zingine kama vile za vituo vya maji na huduma za afya zinatayarishwa kulingana na idadi ya washiriki", iliongeza taarifa hiyo.

# Michezo

Jumapili Novemba 17, 2024

Nipashe




Pogba, Juve wamalizana

UKURASA 22

# Yanga SC yahamishia hasira kwa Al Hilal

## Yaapa italipa kisasi kufuatia machungu...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

SIKU moja baada ya kumtangaza kocha mpya Mjerumani, Sead Ramovic, uongozi wa Yanga umetamba wanajipanga kulipa kisasi katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan itakayochezwa Novemba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara walisema haiwezekani timu yao kufungwa mechi tatu mfululizo na mashindano mbalimbali.**

Yanga imeapa kumaliza hasira za kuondolewa na Al Hilal katika mashindano ya CAF mwaka juzi, lakini pia ikitaka kurejesha furaha kwa mashabiki wao ambao wanaugulia kufuatia kuruhusu kufungwa bao 1-0 na Azam na kichapo cha magoli 3-1 kutoka kwa Tabora United, mechi zote za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza jijini jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe alisema kitendo cha kufungwa mara mbili kimewahuzunisha wanachama, mashabiki na wapenzi wa klabu yao, hivyo kwa vyovyote hawawezi kukubali kupoteza mechi nyingine ya tatu lakini ya kwanza kwenye hatua ya makundi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

“Tumepoteza mechi mbili mfululizo, hatutakubali tena kupoteza mchezo mwingine wa tatu. Huu ni mchezo muhimu kwetu, ni lazima tushinde turudi kwenye njia yetu tulioizoea, hatuwezi kukubali klabu kubwa kama Yanga ifungwe michezo mitatu mfululizo kwa sababu kizazi chetu kitakuwa kimeingia katika rekodi mbaya sana tangu kuanzishwa kwa klabu hii,” alisema Kamwe.

Ofisa huyo aliongeza chini ya kocha mpya wanatarajia mambo mazuri na Yanga haitasikiliza ‘kelele’ za wachambuzi kufuatia uamuzi wake wa kuachana Miguel Gamondi.

“Hautasikia uongozi wa Yanga unajibu lolote kuhusiana na uamuzi wa kuachana na Gamondi, yalisemwa mengi wakati tunaachana na Nabi (Nasreddine), tuliambia tumeleta kocha ambaye alikuwa hana kazi kwa miezi sita.


Angalieni (German mashine-Ramovic), ameondoka kwa sababu gani, tunaendelea na mipango yetu ili kufikia malengo, tunatakiwa kuwa na mbinu mpya pale ambapo timu inahitaji kusonga mbele, tumeshatwaa ubingwa mara tatu, sasa tunataka kuendelea hadhi hii, ni lazima tuje tofauti,” alisema Kamwe.

Aliongeza kocha huyo mpya ameshakutana na wasaidizi wake tayari kuanza mipango kwa ajili ya kuelekea mechi yao ya kimataifa na wanawaomba mashabiki wafike uwanjani wakiwa wamevalia jezi mpya ambazo zinatarajiwa kuzinduliwa Jumatano.

“Kocha wetu baada ya kutangazwa hapo jana (juzi) aliita kikao na wasaidizi wake, Mjerumani huyu hana kupoa kafika tu kataka kikao kingine kwa ajili ya kuhakikisha tunakwenda sawa kwenye maandalizi ya timu yetu kuelekea mechi dhidi ya Al Hilal.

Nitumie fursa hii kuwaambia

INAENDELEA UK. 23



# Mpanzu aongeza nguvu Simba CAF

**Na Adam Fungamwango**

WINGA, Ellie Mpanzu aliyesajiliwa na Simba akisubiri dirisha dogo la usajili litakalofunguliwa Desemba 20, mwaka huu, pamoja na kipa aliyekuwa majeruhi, Ayoub Lakred, walishuka dimbani kwa mara ya kwanza wakati timu hiyo ikicheza mchezo wa kirafiki dhidi ya KMC jijini, Dar es Salaam juzi.

Katika mchezo huo ambao mashabiki hawakuruhusiwa kuingia kwenye Uwanja wa KMC Complex, kwa mara ya kwanza Mpanzu alionekana kuvaa jezi nyekundu na nyeupe, mechi hiyo ikimalizika kwa sare ya bao 1-1.

Mashabiki wa Simba ambao walikuwa nje ya uwanja, na wengine wakichungulia kwa njia sizizo rasmi, walionekana kufurahishwa kumwona winga huyo ambaye alikuwa akiichezea klabu ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo).

Awali, Mpanzu, alikuwa asajiliwe na Simba kipindi cha dirisha kubwa, lakini dili liliharibika baada ya kwenda kufanya majaribio katika Klabu ya Genk ya Ubelgiji, majaribio ambayo hayakufanikiwa.

Baada ya kutofanikiwa na kumaliza mkataba wake wa AS Vita, Simba ilirejea katika meza ya mazungumzo na mchezaji huyo, ikampa mkataba haraka kabla ya dirisha dogo ili kuepuka kuvunjika tena kwa mchakato huo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema baada ya kuichezea kwa mara ya kwanza, Mpanzu ataanza kuitumikia timu hiyo katika mashindano rasmi kuanzia Desemba 18, mwaka huu wakati Wekunsu wa Msimbazi itakapocheza mechi ya raundi ya tatu ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia, utakaopigwa, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Lakini pia anatarajiwa kuonekana kwa mara ya kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara itapokutana na KenGold kutoka Mbeya, mechi ikipanga kufanyika Desemba 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex.

Mbali na winga huyo Mkongomani, pia katika mechi ya juzi alionekana kwa mara ya kwanza, aliyekuwa kipa namba mmoja msimu uliopita, Lakred, raia wa Morocco.

Kipa huyo hakuonekana msimu huu kutokana na majeraha aliyoyapata akiwa katika kambi ya timu hiyo nchini Misri ilipokuwa ikijiandaa na msimu mpya wa mashindano.

Kutokana na kuumia kwake, mabosi wa Simba haraka walimsajili kipa raia wa Guinea, Moussa Camara ambaye kwa sasa ndiye

INAENDELEA UK. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >